SportPesa
TZS. 667,771,400
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Watanzania** 26,000 waugua corona, 725 wapoteza maisha

UKURASA 2



**Gerrard, Terry, Lampard watajwa Aston Villa**

UKURASA 23


# Nipashe

Alhamisi Novemba 11, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580761

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Mwendo wa madumu

• **Mgawo** wa maji wang'ata, Waziri ataja mbinu za kumaliza tatizo... *Ukurasa 2*



Wakazi wa Mtaa wa Sisi kwa Sisi, Manzese, mkoani Dar es Salaam, wakiweka madumu kwenye foleni kwa ajili ya kusubiri kukinga maji yatakapotoka, kutokana na kuwapo kwa mgawo wa huduma hiyo ulioanza hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Balozi Marekani atamani mwafaka kisiasa Tanzania

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Misri, Abdel Fattah Al Sisi, wakikagua gwaride maalum la Jeshi la Misri, baada ya kuwasili Ikulu jijini Cairo, nchini humo jana. **PICHA: IKULU**

## Rais Samia ataja manufaa uhusiano Tanzania na Misri

UKURASA 2

**MICHEZO** **STARS: SAFARI KOMBE LA DUNIA LEO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza wakati akifungua mkutano wa 25 wa Taasisi ya Utafiti Tanzania (REPOA), jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwendo wa madumu Dar es Salaam

**Na Waandishi Wetu**

NI mwendo wa madumu! Ndicho kinachoonekana kwenye baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam kutokana na uhaba wa maji uliotokana na kuwapo kwa mgawo wa huduma hiyo ya msingi.

Jana Nipashe ilishuhudia katika baadhi ya maeneo ya mkoa huo wa kibiashara wananchi wakiwa na madumu, wakitafuta maji kwenye maeneo yanakouzwa.

Mathalani, maeneo ya Kimara maji yalikuwa yakiuzwa kwa Sh. 200 kwa dumu la lita 20, Tabata yaliuzwa kati ya Sh. 200 na 500 kwa dumu, Mbezi yaliuzwa kati ya 300 na 400 kwa dumu, Makumbusho Sh. 500 kwa dumu, Gongo la Mboto yaliuzwa kati ya Sh. 300 na 500 kwa dumu, Buguruni Sh. 500 kwa dumu na Kinondoni yaliuzwa kati ya 300 na 500 kwa dumu.

Wakati hali ikiwa hivyo, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amekiri kuwapo kwa mgawo wa maji mkoani humo, akisema serikali inapanga kutumia chanzo cha maji ya Mto Rufiji kukabili mgawo wa maji ulipo hivi sasa katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Aweso alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya sekta ya maji katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameiagiza wizara hiyo kuhakikisha inalifanyia kazi tatizo la upatikanaji wa maji salama katika Mkoa wa Dar es Salaam.

"Tatizo la mgawo wa maji katika Jiji la Dar es Saalam litaondolewa kwa kutekeleza mradi huu wa kutoa maji katika Bonde la Mto Rufiji na kuyapeleka Dar es Saalam ili kuviongezea nguvu vyanzo vingine vinavyotumika hivi sasa," alisema Aweso.

Alisema kukamilika kwa mradi huo wa Rufiji kutasaidia kuondoa kero ya mgawo wa maji katika Mkoa wa Dar es Saalam moja kwa moja, huku akibainisha hatua zingine wanazozitumia kukabiliana na uhaba wa maji mkoani humo ni kusitisha utoaji wa vibali vya umwagiliaji katika kipindi hiki ambacho kuna ukame.

**UPOTEVU WA MAJI**

Waziri huyo alisema moja ya kero ambayo bado inazikabili mamlaka za maji na usafi wa mazingira ni pamoja na upotevu wa maji kwa kiasi kikubwa.

Alisema kiwango cha upotevu wa maji kinachokubalika ni asilimia 20 tu na siyo vinginevyo, hivyo kama kuna eneo yanapotea zaidi ya kiwango hicho basi kinatokana na wizi.

"Kama kuna eneo kuna upotevu wa maji zaidi ya asilimia 20, basi hiyo inatokana na baadhi ya watu kutokuwa waaminifu ambao wamekuwa wakiunganishia watu maji kinyume na utaratibu katika maeneo kama hoteli na viwanda," alisema Aweso.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika, wastani wa wakazi wa mijini wanaopata huduma ya majisafi na salama imeongezeka kutoka asilimia 25 ya wakazi wote wanaoishi mijini mwaka 1961 hadi kufikia wastani wa asilimia 86 mwaka 2021.

Waziri huyo alisema kikwazo kikubwa katika sekta ya maji ni uhitaji mkubwa wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji, hivyo kuna haja kulinda na kutunza miundombinu ili iendelee kutoa huduma endelevu kwa wananchi mijini na vijijini.

■**Imeandikwa na Paul Mabeja (DODOMA) na Maulid Mmbaga (DAR)**

# Rais Samia ataja manufaa uhusiano Tanzania na Misri

**Na Salome Kitomari**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema mazungumzo yake na Rais wa Misri, Abdel Fattah el-Sisi, yalijikita kwenye ushirikino wa nyanja mbalimbali katika kuimarisha uchumi wa nchi hizo.

Alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari Ikulu nchini humo katika siku ya kwanza ya ziara yake ya siku tatu ambayo ilikwenda sambamba na kutia saini makubaliano kwenye sekta ya elimu na mambo ya nje.

Nyanja hizo ni diplomasia ya kiuchumi, siasa na uhusiano wa kijamii, maendeleo ya ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, umuhimu wa kuimarisha ushirikiano kwenye biashara, utalii na michezo.

Eneo lingine ni ushirikiano kwenye usalama wa nchi hizo, akimshukuru mwenyeji wake kwa msaada wa mafunzo ambao umekuwa ukitolewa kwa vyombo vya usalama nchini.

Kwa upande wa nishati, Rais Samia aliishukuru nchi hiyo kwa kazi nzuri inayofanywa na kampuni mbili za nchi hiyo ya ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere likatalozalisha megawatt 2,150 ambazo zitasaidia ukuaji wa viwanda nchini.

Kuhusu biashara baina ya Tanzania na Misri, Rais Samia alisema imeendelea kukua hasa kwenye uwekezaji na biashara na kwamba biashara baina ya nchi hizo ilikuwa ni Sh. bilioni 84.3 mwaka 2018 na Sh. bilioni 87.3 mwaka 2020 huku ikisajiliwa miradi 26 yenye thamani ya Dola za Marekani Sh. bilioni 1.3 bilioni zilizotoa ajira 2,206.

Rais Samia alisema Tanzania inawakaribisha wawekezaji kutoka Misri kuwekeza kwenye utalii, madini, viwanda, kilimo, majengo, nishati, dawa na usafiri, huku akiahidi serikali itatoa ushirikiano wote kuhakikisha wawekezaji wanafanikiwa.

"Tumekubaliana kufanya kazi kwa pamoja katika kilimo, mifugo na uvuvi kwa Tanzania kupata teknolojia na utaalamu kutoka Misri, pia kwenye uchumi wa bluu tunawakaribisha," alisema.

Rais Samia alisema kwa pamoja waliridhishwa na ushirikinao wa muda mrefu baina ya Tanzania na Misri na kwamba safari yake imeendelea kuimarisha ushirikiano huo uliojengwa na viongozi wa kwanza wa nchi hizo.

"Nimemjulisha Rais, Tanzania tumeendelea kuwa na amani, utulivu na usalama katika nyanja zote kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, hali iliyoiwezesha serikali kuwekeza nguvu kwenye kuboresha huduma za kijamii na kukuza uchumi.

Rais Samia alisema Tanzania imeathiriwa na matokeo ya janga la corona na katika kukabili imewekeza nguvu kuinua sekta muhimu, ambazo ziliathiriwa zaidi kama utalii na wanatarajia ukuaji mzuri, matarajio ya ukuaji wa pato la taifa yakiwa asilimia 5.46 mwaka huu na ujao.

Alisema lugha ya Kiswahili imewaunganisha watu wengi barani Afrika na kuishukuru nchi hiyo kuruhusu lugha hiyo kufundishwa nchini humo, na kwamba watapeleka timu ya wataalamu kuangalia maeneo yenye mahitaji kwa ajili ya maboresho.

Kwa mujibu wa Rais Samia, Tanzania imetia saini mikataba mitatu ya makubaliano na inatarajia watendaji watafanyaka kazi kwa bidii na kuendelea kujadiliana kwa makubaliano mingine yaliyobakia.

Awali, Rais wa Misri, El-Sisi alisema katika mazungumzo yao alieleza namna nchi hiyo itakavyoisaidia Tanzania katika nyanja mbalimbali.

"Tupo tayari kushirikiana na kutoa utaalamu katika kuwajengea uwezo kupitia shirika letu la maendeleo, tutatumia uwezo wetu kuongeza biashara baina ya nchi hizi, ushirikiano wa kisiasa, kuongeza uwekezaji wa Misri Tanzania na kuyafikia masoko, na kumekuwa na ukuaji wa biashara zinazofanywa na Misri nchini Tanzania, hii ni kutokana na ushirikiano wa muda mrefu baina ya nchi hizi," alisema.

# 26,000 waugua corona, 725 wafa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI imesema hadi kufikia Oktoba mwaka huu, idadi ya Watanzania waliothibitika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona tangu ulipoingia nchini ni 26,164 huku 725 wakifariki dunia.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, alibainisha hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee.

Mbunge huyo alihoji: "Tokea janga la ugonjwa wa virusi vya corona lianze, ni Watanzania wangapi wamepata maambukizi, wangapi wamekufa na wangapi wamepona?

"Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa na serikali na zimefanya nini na wapi katika kukabiliana na janga hilo? Je, nini kinapelekea gharama za kupima ugonjwa wa corona kuwa kubwa na ni dawa gani zilizofanyiwa uchunguzi na kuthibitishwa kwamba zina uwezo wa kuzuia au kutibu ugonjwa huo?"

Akijibu maswali hayo, Dk. Mollel alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimeathirika na mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona, akibainisha kuwa hadi kufikia Oktoba 25 mwaka huu, idadi ya Watanzania 26,164 ndio waliothibitika kuwa na maambukizi na kati ya hao 725 walifariki dunia na 25,330 walipona.

Dk. Mollel alisema takribani Sh. bilioni 158 zimetumika kununua vifaa mbalimbali ikiwamo mitambo 19 ya kuzalisha hewa ya oksijeni yenye uwezo wa kuzalisha mitungi 200 hadi 300, kwamba mitambo saba tayari imeshasimikwa na 12 ipo katika hatua ya usimikaji.

Alisema fedha zingine zilitumika kununua vifaa vya kujikinga (PPE), dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi pamoja na magari 105 ya kubebea wagonjwa.

Pia alisema sekta ya afya imepokea Sh. bilioni 466.78 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) ambazo zitatumika katika kupambana na ugonjwa wa virusi vya corona ikiwamo kujenga na kusimika vifaa katika majengo ya matibabu ya dharura (EMD) 115.

Alisema fedha hizo pia zitatumika katika ujenzi wa wodi za uangalizi maalum (ICU) 67, ununuzi wa magari 253 ya kubebea wagonjwa, magari manane ya damu salama, usimikaji wa mitambo 10 ya kuzalisha hewa ya oksijeni, vitanda 2,700 kwenye vituo 225 vya kutolea huduma za afya, kununua na kusimika mashine 95 za X Ray, CT Scan 29, mashine nne za MRI pamoja na kufanya utafiti kuhusu tabia ya virusi vya corona.

Naibu waziri huyo alisema gharama halisi ya kumpima mgonjwa mmoja ni Dola za Marekani 135 na serikali kwa sasa inatoza Dola 50, hivyo serikali inachangia Dola 85.

Kuhusu dawa ya kutibu ugonjwa wa virusi vya corona, Dk. Mollel alisema utafiti mbalimbali umefanyika duniani kuhusu dawa ila hadi sasa dawa zilizopo zinatumika kutibu tu madhara yatokanayo na virusi.

Alisema hata hivyo kilichothibitika kwa sasa kusaidia kuondoa vifo vitokanavyo na ugonjwa wa virusi vya corona ni chanjo.

HABARI KITAIFA

# Balozi Marekani atamani mwafaka kisiasa Tanzania

**Na Richard Makore,** MWANZA

BALOZI wa Marekani nchini Tanzania, Dk. Donald Wright (pichani), amesema anatamani kuona serikali inafanya mwafaka wa kisiasa na vyama vya siasa nchini kama ilivyofanyika visiwani Zanzibar miaka ya nyuma.

Dk. Wright amesema nchi yake inatambua umuhimu wa kuwapo demokrasia Tanzania na kwamba maridhiano yanaweza kuondoa tofauti zilizopo.

Alisema hayo jana jijini hapa, katika mkutano na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kutembelea ofisi za Chama cha Waandishi wa Habari mkoani Mwanza (MPC).

Alisema miaka ya nyuma nchi yake iliweka nguvu nyingi na kuhakikisha mwafaka wa kisiasa visiwani Zanzibar unapatikana na kwamba Tanzania Bara inaweza kutumia mfano huo ili kudumisha demokrasia nchini.

"Miaka ya nyuma tulisaidia ule mwafaka wa Zanzibar kati ya Maalim Seif na CCM na kukapatikana mwafaka wa kisiasa na naamini mfano huo unaweza kutumika pia huku bara," alisema.

Alisema tayari amekutana na vyama vya siasa pamoja na CCM kule Zanzibar na kufanya nao mazungumzo na anaamini kuona mabadiliko katika suala la demokrasia nchini. Akijibu swali kuhusu mtazamo wake wa hali ya demokrasia nchini, alisema imeshuka kidogo ingawa imeanza kupanda tofauti na siku za nyuma kidogo.

Kuhusu uhuru wa vyombo vya habari, Balozi huyo alisema kwa sasa vimeanza kupata matumaini mapya.

Alisema vyombo vya habari vimeanza kuwa huru pamoja na taasisi zingine za haki za binadamu.

"Vitu vyote havitaweza kubadilika kwa siku moja, lakini naona kuna matumaini makubwa ya kuwapo mabadiliko katika vyombo vya habari," alisema.

Alisema ameshakutana na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Tekonolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji na kufanya naye mazungumzo na kwamba alionyesha kutaka kufanya mabadiliko katika sekta ya habari nchini.

Vile vile, alisema waziri huyo ametoa fursa kwa vyombo vya habari kuainisha vikwazo mbalimbali vinavyowakwamisha na kuviwasilisha kwake hadi kufikia Novemba 15, mwaka huu. Dk. Wright alisema majadiliano ni kitu muhimu katika kufikia mwafaka na Dk. Kijaji ameonyesha dhamira njema katika hilo.

Kuhusu masuala ya utafiti wa magonjwa nchini, Dk. Wright alisema nchi yake ipo tayari kusaidia watafiti ili waweze kufanya utafiti mbalimbali wa magonjwa ikiwamo saratani.

Aliwaambia waandishi wa habari, utafiti ni muhimu na Serikali ya Marekani itaendelea kuwasaidia Watanzania wanaotaka kufanya utafiti katika magonjwa mbalimbali.



Pia, alisema Marekani inatoa fedha katika nchi za Afrika kwa ajili ya kufanya utafiti hususani wa ndani za nchi zao wenyewe.

Alitoa mfano namna nchi yake ilivyopunguza vifo vinavyotokana na saratani kwa asilimia 30 mpaka 50.

Alisema mafanikio hayo yalitokana na utafiti uliofanywa kwa ugonjwa wa saratani na walipata matokeo chanya katika eneo hilo.

"Marekani kuna kitengo kinachoitwa National Institute for Health ambacho ndicho kinatoa fedha za kufanya utafiti unaohusiana na magonjwa kama haya," alisema.

Alisema kabla ya kuja nchini kitengo hicho kiliomba kukutana naye ili waweze kuzungumza jinsi wanavyoweza kutoa misaada kwa nchi anayokwenda kufanyakazi.

# Mvutano mwingine mawakili kupinga kupokewa kielelezo

**Na Kulwa Mzee**

WAKILI Peter Kibatala na jopo lake, wameingia katika mvutano mwingine wakipinga kielelezo kupokewa, huku wakitoa sababu saba na kusababisha jopo la mawakili wa Jamhuri kuomba mapumziko ya nusu saa ili warudi kujibu hoja.

Mvutano huo ulitokea jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga, wakati kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, na wenzake watatu ilipokuwa inasikilizwa.

Kabla ya kesi hiyo kuanza, Wakili Kibatala alimtambulisha wakili mwingine kutoka Shinyanga, Paul Kaunda, aliyeungana nao kuongeza nguvu.

Shahidi wa kwanza wa Jamhuri katika kesi ndogo Mrakibu wa Polisi (SP), Jumanne Malangahe kwa kuongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando alidai Agosti 5, 2020 akiwa na askari wenzake wanne kwa kuongozwa na ASP Ramadhan Kingai, waliwakamata mshtakiwa Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya maeneo ya Rau Madukani saa saba mchana.

Alidai baada ya kuwakamata waliendelea kumtafuta mshtakiwa mwingine, Moses Lijenje maeneo mbalimbali ya Moshi mjini, KCMC, Rau Madukani, Pasua, Himo, Aishi Hoteli, Boma na Arusha Sakina. Shahidi alidai maeneo yote hayo hawakufanikiwa kumpata na kurudi Kituo cha Polisi Moshi na Agosti 6 walipokea maelekezo ya kuwapeleka watuhumiwa Dar es Salaam.

SP Jumanne alidai waliondoka Moshi saa moja jioni kuelekea Dar es Salaam ambako walifika alfajiri Kituo Kikuu cha Polisi na kuwakabidhi watuhumiwa mahabusu.

"Tuliwapeleka Dar es Salaam kwa sababu jalada lao lilifunguliwa huko na aina ya uzito wa tuhuma zilizokuwa zinawakabili tulitakiwa kwa namna yoyote ile kuzuia uhalifu uliokuwa unataka kufanyika.

" Tuliwakabidhi kituoni Agosti 7, 2020 wakiwa na hali nzuri kwa mujibu wa mafunzo yetu, Ling'wenya alikuwa vizuri kuanzia kituoni Moshi na kwamba angekuwa na tatizo asingepokelewa," alidai SP Jumanne.

Alidai saa moja asubuhi alitafuta chumba kwa ajili ya kumhoji Ling'wenya na kilipopatikana aliienda kumtoa mahabusu na kumpeleka chumba cha mashtaka kwa ajili ya kuchukua maelezo ya onyo.

Kidando alimuhoji shahidi endapo kitabu cha kuweka kumbukumbu za watuhumiwa wanaoingia na kutoka kituoni kama akikiona atakitambua.

Shahidi alidai atakitambua sababu kuna saini yake katika sehemu iliyoandikwa out, Wakili Kidando aliomba kitabu hicho kipokelewe mahakamani kwa utambuzi.

Wakili wa utetezi, Jeremiah Mtobesya, alipinga kitabu hicho kupokelewa kwa sababu shahidi hajasema tangu aachane na kielelezo hicho Agosti 7, 2020 alikiona tena lini.

Mtobesya alidai shahidi hajaonyesha kama kitabu hicho kinatoka Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam na mwonekano wake ni upi.

Alidai shahidi hajaonyesha msingi, kitabu hicho kimemfikiaje jana na si shahidi sahihi wa kutoa kielelezo hicho kwa utambuzi. Wakili Kibatala alidai anapinga kupokelewa hata kama utambuzi.

Aliendelea kudai kutoa kielelezo hicho mahakamani ni suala la kisheria na kwamba nyaraka hiyo ilitolewa katika shauri dogo la mshtakiwa wa pili Adamu Kasekwa.

Baada ya hoja hizo mawakili wa Jamhuri waliomba mapumziko wakajipange kujibu hoja za mawakili wa utetezi.

Wakili Kibatala alidai hawana pingamizi isipokuwa mapumziko yasizidi nusu saa, maombi hayo yalikubaliwa, Jaji Tiganga aliahirisha kesi hiyo kwa nusu saa.

Akijibu hoja Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdallah Chavula, alidai hawakubaliani na pingamizi la upande wa utetezi na kwamba kanuni za kutoa nyaraka kwa utambuzi au kielelezo ni zilezile.

Alidai moja ya sababu ya kutupilia mbali kesi ndogo ya Adamu Kasekwa iliyokuwa mbele ya Jaji Kiongozi, Mustapha Siyani, alisema ameshangaa kwanini mawakili wa utetezi hawakupinga hicho kielelezo kupokelewa, sio kupinga bali kinakataliwa.

Chavula alidai shahidi anasema alipopewa mtuhumiwa aliweka sahihi katika kielelezo ambacho kinatakiwa kipokelewe na baada ya sahihi aliondoka na mtuhumiwa.

Wakili Mwandamizi, Pius Hillar, akiongezea hoja alidai shahidi wa Jamhuri ana taarifa ya tukio lililotokea Agosti 7, 2020.

"Hoja zetu kwenye hili ni kwamba wenzetu hawako sawa sawa, kwa sababu mahakama yako mheshimiwa jaji haijaelezwa ni sheria na utaratibu upi umekiukwa.

"Ushahidi huo ni msingi tosha kwamba shahidi anazungumzia nyaraka ya kitu gani, hoja za mawakili wa utetezi haziwezi kuzuia nyaraka kupokelewa, hoja zao hazina uzito tunaomba pingamizi litupiliwe mbali."

Wakili Paul Kaunda akiongezea nguvu katika hoja za utetezi, alidai muda pekee wa kupinga nyaraka inayowasilishwa mahakamani iwe kwa maombi ya utambuzi au kielelezo ni pale inapotolewa.

"Shahidi hajaiambia mahakama nini kilitokea kuanzia Agosti 7, 2020 mpaka sasa kuhusu kitabu hicho, alipaswa asiache ombwe," alidai Kaunda.

Mawakili pande zote mbili walimaliza kuwasilisha hoja wanasubiri uamuzi wa mahakama wa kukubali hoja za utetezi au kutupilia mbali hoja hizo.

# IGP apangua makamanda

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, amefanya mabadiliko na kuhamisha baadhi ya makamanda wa polisi wa mikoa na kuwapandisha wengine.

Taarifa ya jeshi hilo iliyotolewa jana na Msemaji wake, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) David Misime, iliwataja waliohamishwa ni Kamanda wa Polisi wa Iringa, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Juma Bwire, anayehamishiwa Makao Makuu ya Polisi Kamisheni ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai.

Misime alisema nafasi yake inakuchuliwa na Ofisa Mnadhimu wa Mkoa huo, ACP Allan Bukumbi.

"Aliyekuwa Mkuu wa Operesheni Kanda Maalum ya Dar es Salaam, ACP Ali Mohamed, amehamishiwa Mkoa wa Katavi kuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo akichukua nafasi ya Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamin Kuzaga ambaye amehamishwa kwenda kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara," alisema.

Misime aliwataja wengine kuwa ni aliyekuwa Kamanda wa Polisi wa Manyara, Marisone Mwakyoma, amehamishiwa Dodoma kuwa Msaidizi wa Ulinzi wa Miundombinu Muhimu ya Serikali na ACP Zuberi Mwombeji ambaye sasa anakuwa Mkuu wa Operesheni Kanda Maalum ya Dar es Salaam," alisema.

Misime alisema uhamisho na mabadiliko hayo ni ya kawaida wenye lengo la kuboresha ufanisi katika kutekelezaji wa jukumu la kulinda maisha ya watu na mali zao.


## NOTISI / TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, ,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA MBILI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | FOREST MBEYA NA TUNDUMA | 25/11/2021 SAA TANO ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | TAMIKA IZACK MWALUMU | NYUMBA | TAMIKA IZACK MWALUMU | TABATA KINYEREZI | 04/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | VIP PRODUCTION AND SUPPLY | NYUMBA | HASANI HASANI MUMBI | MAJOHE | 03/12/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | BENARD KEMBO NDIEGE | NYUMBA | BERNAD KEMBO NDIEGE NA ASHURA SAID MCHOPA | KIGAMBONI | 30/11/2021 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0754497396/0674821287/0755506970
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

*2165648O2*

# Sakata kusuasua kukamilika Bwawa la Nyerere laibua mjadala bungeni

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

MJADALA wa kuchelewa kukamilika kwa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), umeibuka bungeni huku Mbunge wa Viti Maalum, Ester Bulaya (Pichani), akiliomba Bunge kuiagiza serikali kuwasilisha bungeni taarifa ya maendeleo ya miradi yote ya kimkakati.

Juzi, wakati wa mjadala wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23, Bulaya alitaka maelezo ya serikali juu ya maendeleo ya mradi wa JNHPP, akidai kuwa mradi huo hadi sasa umefikia asilimia 45, nyuma ya makubaliano ya mkataba unaopaswa kufikia asilimia 98 kwa sasa.

Bulaya alisema: "Status (hali) ya Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ikoje? Kwa taarifa nilizo nazo mradi umefikia asilimia 45 na hadi sasa ulipaswa kufikia asilimia 99, leo ni siku ya 834".

"Ujenzi wa tuta hadi sasa ni asilimia 43, wakati leo ilipaswa kuwa asilimia 88. Njia ya kupokelea maji kwenye mitambo sasa hivi iko asilimia 57, ilipaswa iwe asilimia 94. Kituo cha kupokea na kusafirisha umeme hadi sasa kimekamilika kwa asilimia 50 wakati ilipaswa kuwa asilimia 99, hii ni kinyume na mkataba.

"Ni lazima tuambiwe, na kuna taarifa kwamba mradi huu unazidi kwenda mbele zaidi kuliko makubaliano ya mkataba. Lazima tuambiwe, kuchelewa kukamilika kwa mkataba kwa wakati, serikali itamtoza mkandarasi kiasi gani kwa siku," aliongeza.Kutokana na hoja hiyo, ilimlazimu Mbunge wa Nzega Vijijini, Hamisi Kigwangala, kumpa taarifa Bulaya.

Kigwangala alisema mradi huo umechelewa kukamilika kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali, zikiwamo za kimazingira, ambazo zilisababisha kuweka sawa majadiliano kati ya serikali na wadau wa mazingira.



Sababu ya pili, alisema ni mlipuko wa ugonjwa wa corona ambao ulisababisha baadhi ya mitambo kuchelewa kuingia nchini kutokana na viwanda vingi duniani kufungwa.

**MAJIBU YA SERIKALI**

Akitoa ufafanuzi wa suala hilo, Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema ni kweli kulikuwa na changamoto katika mradi huo ambazo ni za kawaida na kwamba hazitakwamisha kuendelea kwa mradi huo.

Alisema serikali ilishachukua hatua katika maeneo yalikuwa na uzembe kwamba mazungumzo yanaendelea kati ya serikali na mkandarasi ili kufidia siku 477 zilizopotea.

"Zoezi (kazi) la (ya) kujaza maji katika bwawa hilo litachelewa (itachelewa) kuanza kutokana na mkandarasi kuchelewa kuziba handaki alilochimba kuchepusha maji," alisema.

"Kuchelewa huko ni jambo la kawaida katika utekelezaji wa miradi mikubwa, hata hivyo TANESCO pamoja na Wizara ya Nishati wameanza kuchukua hatua dhidi ya watendaji waliohusika na ucheleweshwaji wa mradi huo," aliongeza. Alisema mkataba huo uko wazi na umeweka utaratibu wa hatua za kuchukua ikiwa itatokea kuna ucheleweshwaji wa mradi.

"Hivyo tunakaa na mkandarasi kuhakikisha kuwa tunapunguza siku zilizocheleweshwa, kuzuia ucheleweshwaji zaidi na pia kuhakikisha hakuna ongezeko la gharama ya mradi," alisema Makamba.

Waziri Makamba alisema ili bwawa hilo la kufua umeme lianze kujazwa maji ni sharti liwe limejengewa tuta lenye urefu wa 190 kutoka usawa wa bahari kazi ambayo tayari imesha kamilika.

Alisema pia inapaswa kuhakikisha linazibwa handaki lililojengwa kuchepusha maji ya mto, pamoja na kuwapo kwa milango mikubwa ya chuma ilikuzuia maji kuendelea kupita njia mpya.

# Mpango ahimiza utafiti wa viwanda

**Na Beatrice Shayo**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewataka watafiti nchini kufanya utafiti utakaoonyesha jinsi viwanda vinavyoweza kukua kutoka vidogo na kufikia vikubwa

Dk. Mpango alitoa ushauri huo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya miaka 25 ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Kupunguza Umasikini nchini (REPOA) iliyowakutanisha watafiti na wadau mbalimbali.

Alisema kuna umuhimu wa kufanyika kwa utafiti wa kujua kwa lengo la kuvibadilisha viwanda vidogo viwe vya kati ili kuongeza uzalishaji.

Alisema Tanzania ina jumla ya viwanda 8,477 asilimia 92 ni viwanda vidogo au vidogo zaidi, asilimia 5.4 ni vya kati na asilimia 2 ni vikubwa.

Dk. Mpango alizitaka Taasisi na watafiti wengine kufanya tathmini ya mnyororo wa thamani wa mazao ya kimkakati, bidhaa na madini ili wananchi pamoja na serikali wanufaike na mnyororo huo.

Alisema Tanzania ni nchi kubwa yenye rasilimali nyingi, lakini mnyororo wake wa thamani haujaendelezwa na bidhaa nyingi zinasafirishwa nje ya nchi zikiwa ghafi, hali ambayo inachangi kuikosesha nchi mapato.

Aidha, Dk. Mpango aliagiza utafiti kwenye sekta isiyo rasmi kwa kuwa Watanzania wengi wanaendesha shughuli zao katika mfumo usio rasmi, hali inayosababisha uzalishaji hafifu na upotevu wa mapato.

Alisema ipo haja kuangalia mkakati gani ifanyike kuhakikisha Watanzania wengi wafanye kazi zao katika uchumi rasmi.

Aidha, Dk Mpango alisema serikali itafanyia kazi maoni ya kitafiti kwenye maeneo na imejikita kuboresha miundombinu ili kukuza uchumi wa nchi.

Naye Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, alisema serikali inathamini shughuli za utafiti kwa sababu ni nyenzo muhimu katika kufanya uamuzi/

Alisema Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo umejengwa katika uchumi wa viwanda kwa sababu na serikali inatakiwa kupiga hatua kiuchumi. Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk, Donald Mmari, alisema katika kipindi cha miaka 25, Taasisi hiyo imeweza kuwajengea uwezo watafiti, watumishi wa serikali, asasi za kiraia zaidi ya 3,000 nchi nzima.

Alisema REPOA imekuwa ni taasisi inayokua na utafiti unaofanywa kila mwaka na Programu ya Taasisi za Utafiti na za Kiraia ya Chuo Kikuu cha Pannyslvania nchini Marekani uliitaja REPOA kama taasisi bora ya utafiti nchini kwa miaka sita mfululizo na ya nne Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Alisema wanaamini utafiti katika maeneo mbalimbali utaendelea kutoa majibu ya matatizo ili Tanzania iweze kujenga uchumi na kufikia malengo yake.


CCBRT
COMPREHENSIVE COMMUNITY BASED REHABILITATION IN TANZANIA

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**CCBRT** inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 401 AKL – TOYOTA LANDCRUISER.** Chassis namba **JTER87IJ700024986.** Engine namba **IHZ0470578.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 405 AKL – TOYOTA LANDCRUISER.** Chassis namba **JTER87IJ000026011.** Engine namba **IHZ0470721.** ***Magari hayo yalikuwa yamesajiliwa kwa majina ya Christian Social Services Commission (CSSC) na ambayo kwa sasa yanamilikiwa na Hospitali ya CCBRT iliyoko Msasani Dar es salaam.*** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DAR/MBU/RB/836039/2021.**

216565802


# Mbaroni madai ya kuiba mtoto

**Na Christina Haule,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linamshikilia Maria Zayumba (28), mkazi wa Sangasanga, kwa tuhuma za wizi wa mtoto wa kike mwenye umri wa miaka sita (jina linahifadhiwa).

Zayumba anadaiwa kumwiba mtoto huyo wa darasa la kwanza (shule inahifadhiwa) na kumsafirisha kwenda mkoani Iringa ili kumridhisha mume wake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilimu, alisema jana kuwa Zayumba alikamatwa Novemba 8, mwaka huu, majira ya saa 7:00 mchana kwenye maeneo ya Soko Kuu la Chifu Kingalu lililoko Kata ya Mji Mkuu, Manispaa ya Morogoro.

Kamanda Musilimu alisema mtuhumiwa huyo anadaiwa kumwiba mtoto huyo tangu Oktoba 22, mwaka huu, alipokuwa akirejea nyumbani kwao kutoka shuleni baada ya kumrubuni kuwa anampeleka nyumbani kwao.

Alisema mtuhumiwa huyo badala ya kumpeleka nyumbani kwao mtoto kama alivyomwahidi, aliamua kumsafirisha hadi mkoani Iringa kwa lengo la kujifanya kuwa ni mwanawe ili kumridhisha aliyekuwa bwana au mume wake.

Kamanda Musilimu alisema awali, Oktoba 23, mwaka huu, mama mzazi wa mtoto huyo alitoa taarifa ya kupotelewa na mtoto kwenye Kituo Kikuu cha Polisi Morogoro na kupewa RB namba MOR/RB/9089/2021 na kuendelea kumtafuta juhudi ambazo hazikuwa na mafanikio.

Alisema Novemba 8, mwaka huu, majira ya saa 7:00 mchana, polisi walipokea taarifa ya kuonekana kwa mtoto huyo kutoka kwa mama mmoja ambaye ni jirani yao aliyemwona mtoto akiwa na mama mwingine ambaye hamfahamu.

Alisema inadaiwa kuwa mama huyo jirani alimfuata mama aliyekuwa na mtoto na kumuuliza uhusiano wake na mtoto huyo kwa sababu yeye alikuwa na taarifa za kupotea kwa mtoto huyo na anatafutwa na wazazi wake. Kamanda huyo alisema mama aliyekutwa na mtoto hakuwa na majibu ndipo wananchi walimdhibiti na kutoa taarifa polisi. Alisema polisi walikwenda na kumchukua kisha kumpeleka kituo kikuu cha polisi akiwa na mtoto aliyemwiba kwa hatua zaidi za kisheria. Baadaye mtoto alikabidhiwa kwa wazazi wake ili aendelee kupata malezi bora ikiwamo elimu.

Alisema Jeshi la Polisi kupitia dawati la jinsia na watoto linaendelea kumhoji mtuhumiwa kuhusiana na tuhuma za wizi wa mtoto na upelelezi utakapokamilika atafikishwa mahakamani.

HABARI KITAIFA

# Tril. 8/- zahitajika kukamilisha upelekaji umeme kila kitongoji

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA



WAZIRI wa Nishati, January Makamba, (pichani) amesema Sh. trilioni nane zinahitajika ili kuuwezesha Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kupeleka huduma ya umeme katika kila kitongoji nchini.

Amesema hadi kufikia mwaka 2024 mikoa yote nchini itakuwa imeunganishwa katika gridi ya taifa.

Makamba alitoa taarifa hiyo bungeni wakati akijibu hoja za wabunge wakati wa mjadala wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka 2021/22. Wabunge walihitaji kufahamu mikakati ya serikali katika kuhakikisha huduma ya umeme inafika katika vijiji vyote nchini.

Makamba alikiri kwamba kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vyote nchini imechelewa kufikia kila kitongoji kwa sababu kulikuwa na changamoto ya takwimu ya kufahamu wapi kijijini na wapi si kijijini.

"Tunakuja na mradi mkubwa. Tunafahamu umeme hautumiwi na kijiji unatumiwa na watu, Wizara inataka kuainisha mahitaji halisi ili watakaohitaji umeme waweze kubainishwa na kuunganishwa katika ngazi ya kitongoji," alisema.

Makamba alisema kwa takwimu zilizopo, Tanzania inakadiriwa kuwa na vitongoji 64,384 lakini ni vitongoji 27,000 tu ndivyo vilivyofikiwa na nishati ya umeme.

Waziri alisema wizara yake inakusudia kuwaleta makandarasi wa umeme wanaotekeleza miradi ya umeme nchini kufika bungeni Februari mwakani, ili kufanya mawasiliano ya moja kwa moja na wabunge.

"Tunatengemea kuwa makandarasi hao watatumia siku tatu na mbunge atakuwa na mawasiliano ya moja kwa moja kubainisha maeneo ambayo bado yanachangamoto," alisema.

# Waziri: Ubunifu unahitajika kukuza sekta huduma fedha

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema unahitajika ubunifu ili kukuza sekta ya huduma za fedha nchini zilizo rahisi kwa watumiaji hususan wajasiriamali wadogo.

Aidha, imesema kufanya hivyo kutawawezesha Watanzania wote kifikiwa na huduma hiyo.

Kadhalika, mpango wa kutoa elimu kwa umma wa miaka mitano kuanzia mwaka huu hadi 2026, matarajio ni kuelimisha wananchi kuhusu haki zao, na wajibu wa watoa huduma.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango), Zanzibar, Jamal Kassim Ali, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Huduma za Fedha kitaifa, iliyoshirikisha taasisi na kampuni ya bima, mifuko ya hifadhi ya jamii, masoko na dhamana.

Jamal alisema pamoja sekta hiyo kukua, bado kuna vikwazo ikiwamo uhaba wa mikopo kwa wajasiriamali wadogo, huduma kuwafikia Watanzania wachache huku asilimia nane pekee ya waliopo vijijini nchini, hutumia huduma hiyo.

"Baada ya elimu hii wiki nzima, tujipime kwamba ni Watanzania wangapi wameongeza uelewa na elimu ya huduma za fedha kwenye masoko, mitaji wamejiunga wangapi. Sekta hii iboreshwe ili uchumi wa Watanzania ukuzwe na kipato chao nacho kikue," alisema Jamal.

Alisema sekta ya fedha ipo katika makundi tofauti ikiwamo mifuko ya jamii, masoko na mtaji hadi Agosti mwaka huu umeongezeka na kufikia Sh. trilioni 18.6 na vikundi vya fedha ikiwamo Vikoba vimeongezeka.

"Sekta ya fedha imechangia asilimia 3.1 ya pato la taifa mwaka jana. Zimetengwa shilingi bilioni 133 ili kuwawezesha wajasiriamali ambao pia wana haki ya kutumia huduma za kifedha zilizo rasmi, kuwa na bima, kupata mitaji na masoko," alisema Jamal.

Mkurugenzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Festo Fute, alisema kila mwaka hukusanywa Sh. trilioni 3.5 kutoka kwa wanachama wa mifuko hiyo, na kwamba elimu inahitajika ili wastaafu na watumishi wafahamu matumizi sahihi ya fedha wanazopewa na mifuko hiyo.

"Sekta ya hifadhi mifuko ya jamii ina athari katika jamii, hivyo fedha zake inabidi elimu itolewe kuhusu matumizi yake. Pia kunahitajika uhamasishaji sekta binafsi kujiunga," alisema Festo.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatma Nyangasa, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam, aliwataka wakazi wa mkoa huu wajitokeze kupata elimu inayotolewa kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, ili kujua matumizi sahihi na rasmi ya fedha.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA YA KUNUNUA GARI MPYA NA AU KUKODISHA. KUMBUKUMBU: 0010007221**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya kununua gari mpya na au kukodisha.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

Mradi wa EACOP unahitaji watoa huduma wenye uzoefu na uwezo yakinifu wa kutoa huduma ya kununua gari mpya na au kukodisha:

- Magari ya kati (SUV), Magari madogo yenye uwezo wa kubeba abiria 5 ambazo zinaendeshwa kwa mfumo wa Automatic transmisión (makadirio ya idadi kuanzia 30 mpaka 50 kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia sasa).
- Kupatikana kwa magari aina ya Double Cabin 4x4 ambayo yana mfumo wa uendeshaji wa Automatic Transmission (makadirio ya idadi 30 hadi 80 kwa kipindi cha kuanzia sasa mpaka mwaka).
- Kutoa huduma ya matengenezo ya magari husika (Preventive and periodic), kujumuisha usimamizi wa matairi na ubadilishaji wake.
- Kuorodhesha matawi au washirika wake ndani ya Tanzania.
- Kutoa taarifa za gari husika kama zina viwango vya kiusalama vinavyolingana na NCAP.
- Kutoa taarifa ambazo zitaonyesha aina ya gari au modeli ambazo zinapatikana kwa sasa (Stock) na ambazo wanategemea kuingiza nchini katika kipindi cha mwaka ujao.

**VIGEZO MUHIMU:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika mawanda ya kazi, kwa viwango vya juu nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 5 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa watendakazi husika wenye vigezo na uzoefu katika kutoa huduma ya kununua gari mpya na au kukodisha.
- Inashauriwa, muoneesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka uliopita.
- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Afya, Mazingira na Usalama, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani vya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa usajili katika mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacoptz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **25 Novemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe kiwe ni kumbukumbu namba husika tu. Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni **0010007221.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

216563102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuweke mkazo matumizi ya gesi

**JUZI** Wizara ya Nishati ilieleza kuwa katika kipindi cha mwaka 2004 hadi Juni 2020, matumizi ya gesi asilia ya Mnazi Bay na Songo Songo yamesaidia serikali kuokoa zaidi ya Sh. trilioni 38, ambazo zingetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya mitambo ya umeme na ya viwandani.

Aidha, alisema gesi iliyogunduliwa nchi kavu na kina kirefu cha bahari ni futi za ujazo trilioni 57.54 mwaka 2021, ambao umewezesha kuanza kutumika kwa gesi asilia kama chanzo cha nishati hususan kwa uzalishaji umeme, viwandani, majumbani na kwenye magari.

Wizara hiyo ilisema hadi Oktoba 2021 viwanda 52 mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Mtwara vinatumia gesi asilia, huku vituo vya kushindilia na kujaza nishati hiyo kwenye magari kwenye mikoa hiyo vikifanyakazi.

Pia imesema matumizi ya gesi asilia yamesaidia kupunguza utegemezi wa uzalishaji wa umeme kwa kutumia nguvu za maji, na hadi Novemba 2021 takribani asilimia 60 ya umeme unazalishwa kwa kutumia gesi.

Wizara hiyo inaongeza kuwa hadi Machi mwaka huu mapato yatokanayo na mauzo ya gesi yamechangia zaidi ya Sh. bilioni 208 katika mfuko wa mafuta na gesi kuanzia mwaka 2016/17 baada ya kukamilika kwa ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, hadi Desemba mwaka jana, serikali ilipata mapato ya zaidi ya Sh. bilioni 441 yatokanayo na kodi mbalimbali kuanzia mwaka 2015 baada ya kukamilika kwa bomba hilo.

Wakati hali ikiwa hivyo kwenye takwimu, uhalisia ni kuwa asilimia 80 ya Watanzania bado wanategemea nishati ya mimea kwa ajili ya kupikia na shughuli nyingine.

Gesi ilipogundulika nchini ahadi ilikuwa ni kuisambaza kwenye makazi ya watu na wananchi wa Dar es Salaam, Mtwara na Lindi waliahidiwa kusambaziwa huduma hiyo nyumbani, ikiwa ni namna ya kupunguza bei ya nishati, lakini hali haikuwa hivyo.

Pia wananchi wa Mtwara na Lindi walipewa matumaini makubwa kuwa rasilimali hiyo inakwenda kubadilisha maisha yao kwa kuwa mikoa hiyo ingekuwa kama Ulaya au Dubai, kiasi cha kutokea vurugu kutokana na kuamini kuwa wanaporwa mali hiyo na walitaka ibaki huko kwa ajili ya kuwanufaisha wao kwanza kabla ya kuondoka.

Lakini hadi sasa hata wananchi wa mikoa hiyo hawajanufaika na nishati hiyo kwa matumizi ya nyumbani zaidi kwa kupata umeme kwa kuwa hawajaunganishwa kwenye gridi ya taifa.

Ikiwa gesi itawafikia wananchi wengi kwa bei rahisi maana yake watu wataachana na kukata kuni au miti kwa ajili ya mkaa, lakini kwa sasa kuna matumizi makubwa ya mkaa kwa kuwa bado mbadala uliopo haujatosheleza mahitaji.

Ni kweli serikali imeokoa fedha hizo ambazo zingenunua mafuta, lakini mzigo wa maisha uko kwa mwananchi wa kawaida, ambaye bado anatumia mkaa au gesi ya mitungi kwa ajili ya kupikia au shughuli nyingine, ambaye alitarajia kugundulika kwa gesi kungebadili maisha yake.

Katika kipindi hiki ambacho mabadiliko ya tabianchi yanaonekana dhahiri na dalili zikionekana kama jua kali, kipindi kirefu cha kiangazi ambacho husababisha ukame ambao huathiri binadamu, wanyama na viumbe wengine.

Kumekuwa na jitihada za kuhamasisha wananchi kupanda miti kwa wingi, lakini kasi ya kuvuna mkaa ambao husafirishwa kwenda mijini ni kubwa ambako wengi hutumia gesi, mkaa na kuni. Kwa kawaida mti unaoteketezwa sasa ukipandwa mwingine itachukua miaka zaidi ya kumi kuuvuna, maana yake ni lazima kuwa na nishati mbadala na kuachana na kutegemea mimea.

Ni muhimu serikali ikatimiza azima yake ya kuhakikisha taasisi zote za umma hasa elimu na afya zinatumia gesi, ili kuondokana na matumizi ya kuni au mkaa ambayo ni uharibifu wa mazingira, vinginevyo nchi itabaki wazi na athari zitakuwa kubwa kwa wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Tunatamani itimu ndoto gesi kushuka, tuage kwa vitendo matumizi ya mkaa

Na Halfani Chusi

**SERIKALI** kila kukicha inawaza na 'kuwazua' namna ya kuondoa jamii katika matumizi ya mkaa, ili kuepusha ukataji miti ovyo.

Hapa naona serikali ina maono ya mbali sana, japo ili mtu atambue maono ya serikali, anahitaji kufikiria kwa kina, japo nithubutu kuchangia binafsi tutumie fikra kiasi, kuielewa serikali inachomaanisha.

Kwanza, kuna maana kubwa sana pale serikali inapohamasisha watu kuepukana na matumizi ya mkaa na baadala yake watafute njia mbadala. Serikali inaona watu wakiendelea kutumia mkaa maana yake miti itaisha na huku ndio chanzo kikubwa cha mvua na manufaa mengine ya kimazingira.

Hapo kuna ukweli, jamii itakosa hewa safi inayotokana na miti, pale itakapoteketezwa. Kuna baadhi ya miti hutumika kama dawa na kwa hiyo, inapotokea kukatwa, maana yake ni hatari kwa tiba ya umma, hata viumbe vinginevyo.

Ili kuwahamisha watu kutumia mkaa, ni lazima kwanza njia mbadala zitengenezewe ya kuwa na mazingira ya kuwa na gharama ndogo, hata hitaji kumfikia mtu wa ngazi ya chini kumudu hitaji hilo.

Tafsiri yake ni nini? Iwapo bei ya gesi itaendelea kuwa juu mara zote, maana yake haiwezi kumhamasisha mtu aache kutumia mkaa na ahamie katika gesi.

Hapa naona kwanza, serikali kujipanga katika namna ya kuangalia kushusha gharama za gesi na itakapokuwa ya gharama nafuu, kisha kuwa rahisi mtu ataachana na mkaa na baadaye atutumia gesi katika mahitaji yake.

Pale panapotakiwa, ikitokea marufuku ya matumizi ya mkaa wakati gesi bei yake imebaki chini, nadhani hiyo itakuwa njia rahisi kukwamisha matumizi ya mkaa.

Gesi kwa sasa, mtungi mdogo unauzwa hadi Sh.22,000 na lazima mtu mwenye hali ya chini, atakimbilia kwenye mkaa tu na hakuna namna, lakini ingekuwa walau chini ziadi sidhani kama kuna mtu angekimbilia penye mkaa.

Sambamba na kupunguza bei ya gesi, ni lazima pia serikali irahisishie wananchi vyanzo vingine vya nishati kama upatikanaji makaa ya mawe. Hayo nayo yanatajwa sana kuwa njia mojawapo ya kujiepusha na matumizi ya mkaa na kuni.Lakini, tuna haja ya kukiri upatikanaji wake nao ni mgumu, kwa maana hakuna urahisi wa kupata makaa ya mawe kama ilivyo kuni.

Ndipo inapozaa hitaji la serikali kuendelea kuangalia namna ya kurahisisha upatikanaji malighafi hizo ili kupunguza, kama sio kumaliza utumiaji mkaa.

Hilo limemkuna Waziri wa Nchi Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo na kuanza kueleza namna serikali ilivyojipanga kuondoa matumizi ya mkaa, akiwashauri Watanzania waanze kujenga utamaduni wa kutumia njia mbadala, ikiwamo gesi na makaa ya mawe. Jafo amesema hayo, alipoongea na waandishi wa habari katika moja ya mikutano yake, huku akionekana ni mtu anayelipokea suala la matumizi ya mkaa kwa shingo upande, hivyo ikidhihirisha namna waziri hapendezewi na matumizi ya mkaa.

Waziri anatamka: "Tunatamani siku moja kuona tunaachana na suala la matumizi ya mkaa katika nchi yetu. Pia, tunatamani kuwa na kizazi kitakachotumia zaidi nishati jadilifu, kwa sababu matumizi ya mkaa yanasababisha athari nyingi sana katika jamii, ikiwamo uchafuzi wa mazingira na kusababisha mabadiliko ya hali ya hewa na mengine mengi."

Hilo pia, linanisukuma mtaani mwandishi kupata ufahamu wa je, ni kweli jamii inatamani kutumia gesi, lakini inashindwa kwa sababu ya gharama?

Hilo analithibitisha mama muuza chakula, Selina Juma, eneo la Sinza, Dar es Salaam, anayefafanua kuwa:"Sisi 'mama ntilie' tunatamani sana kutumia gesi, kwa sababu ni 'chapchap' upikaji wake. "Lakini tunaona gharama ni kubwa. Kwa hiyo, ukitumia gesi hupati faida ndio maana tunalazimika kutumia mkaa, lakini tunapenda kutumia gesi."

Maelezo hayo matamu yananivuta kusogea mbele mbele kidogo, nakutana na kijana muuza chipsi Ziaka Geda, naye ana ufafanuzi:"Katika biashara ya chipsi, ukitumia gesi hupati faida, ila gharama ikipungua tutaachana na mkaa kabisa kwa sababu hata kiazi chenyewe ukikipika kwenye gesi kinatoka kimenyooka kizuri kuliko hata kwenye mkaa."

■**Mwandishi anapatikana kwa simu: 0787879707**

HABARI KITAIFA

# Mloganzila yawezeshwa vifaa tiba vya mil. 132/-

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, imepokea msaada wa vifaa vya matibabu katika kitengo cha dharura, wenye thamani ya Sh. milioni 132.

Miongoni mwa vifaa vilivyopokewa ni vya kupima umeme wa moyo, oksijeni mwilini mwa mgonjwa, shinikizo la damu, vifaa vya upasuaji na kifaa cha kupoozea damu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Lawrence Museru, akizungumza juzi katika hospitali hiyo baada ya kukabidhiwa msaada huo kutoka kampuni ya Abbott, alisema vitasaidia kutoa huduma bora katika Idara ya Magonjwa ya Dharura na kuongeza utendaji kwa wataalamu wa hospitali hiyo.

"Napenda kuahidi kwamba vifaa tiba hivi vitatumika inavyotakiwa. Pia vitasaidia kuendesha shughuli za matibabu katika Idara ya Magonjwa ya Dharura bila matatizo yoyote," alisema Prof. Museru.

Alisema ushirikiano kati ya Hospitali ya Muhimbili-Mloganzila na Mfuko wa Abbott-Tanzania ulisaidia kuongeza ufanisi katika maeneo mbalimbali ya hospitali hiyo pamoja na Muhimbili-Upanga.

Museru aliongeza kuwa ushirikiano kati ya Muhimbili na Mfuko wa Abbott-Tanzania, una zaidi ya miaka 10 na kwamba umewanufaisha wananchi kwa sababu mfuko huo umekuwa ukitoa msaada wa vifaa tiba katika maabara ya Hospitali ya Taifa Muhimbili-Upanga.

Pia Prof. Museru alisema wana mpango wa kuanzisha masomo ya uzamili ya magonjwa ya dharura nchini. Alisema ushirikiano huo unasaidia pia kujengwa kwa vituo vya kutoa huduma za magonjwa ya dharura katika baadhi ya mikoa nchini pamoja na kujenga jengo la wagonjwa wa nje Muhimbili-Upanga.

Kabla ya kutolewa kwa vifaa hivyo, kitengo hicho kilikuwa kikitumia kifaa kimoja kimoja, vilivyokuwapo, wakati mwingine wakibadilishana na Kitengo cha Wagonjwa walio katika Uangalizi Maalum (ICU).

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Abbott-Tanzania, Dk. Natalia Lebou, aliishukuru Hospitali ya Muhimbili-Mloganzila kwa kushirikiana na Mfuko wa Abbott- Tanzania katika kuboresha huduma za afya nchini.

"Ni kweli tunashirikiana na Muhimbili Upanga na Mloganzila, katika kujenga vituo vya kuhudumia wagonjwa wa dharura nchini pamoja na kusaidia vifaa tiba," alisema Dk. Lebou.




Mkurugenzi wa Kampuni ya JJAD Kagera Farmers (T), Dk. Albert Katagira, akiwa ameshika makombe ambayo kampuni yake ilitunukiwa kwa kushika nafasi ya pili na ya tatu katika uzalishaji wa kahawa bora aina ya robusta kwenye mashindano yaliyoendeshwa na Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), mkoani Kilimanjaro hivi karibuni. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kampuni yashinda tuzo ya kahawa bora 2021

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya JJAD Kagera Farmers (T) Limited, imeshinda tuzo ya kuwa mzalishaji bora wa kahawa nchini kwa mwaka 2021.

Mashindano hayo yaliyoendeshwa na Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), yalifanyika hivi karibuni wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro.

Kwenye mashindano hayo yaliyoshirikisha sampuli 68 za kahawa kutoka mikoa mbalimbali nchini, JJAD iliibuka kidedea kwenye kahawa aina ya Robusta kwenye nafasi ya pili na ya tatu baada ya tathmini kufanyika.

Mkurugenzi Mtendaji wa JJAD, Dk. Albert Katagira, alisema mashindano hayo hufanyika kila mwaka kwa lengo la kuwahamasisha wakulima kuzalisha kahawa bora zaidi.

Alisema kwenye mashindano yaliyomalizika hivi karibuni, ziliwasilishwa sampuli 68 kisha kufanyiwa tathmini ya ubora na wataalamu wa TCB ndipo JJAD iliibuka mshindi kwa upande wa kahawa ya Robusta.

Alisema JJAD ni kampuni inayozalisha na kuuza kahawa nje ya nchi na ina mashamba zaidi ya ekari 100 wilayani Kyerwa mkoani Kagera.

Dk. Katagira alisema katika kuboresha ubora wa kahawa, JJAD imeingia mkataba na TCB kwa ajili ya kuzalisha miche bora ya kahawa aina ya Robusta ambayo ina tija kwa asilimia 100 kulinganisha na miche ya zamani.

Alisema miche hiyo bora inatokana na mbegu bora zilizotoka Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI).

Miche bora ya kahawa wanayozalisha, alisema inaanza kuzalisha kahawa baada ya mwaka mmoja na nusu wakati ile ya zamani huchukua hata miaka minne kuanza kuzaa.

Dk. Katagira alisema mche mmoja wa mbegu bora ya robusta unauwezo wa kuzalisha kilo 2.5 ya kahawa kwa mwaka wakati ile ya zamani uwezo wake ni kuzalisha nusu kilo kwa mwaka.

Alisema mipango yao kwa mwaka 2021 ni kuzalisha miche milioni 1.5 mwaka 2021/22 miche milioni tatu mwaka 2022/23 miche milioni 4.5 mwaka 2023/24 miche milioni sita na mwaka 2024/25 miche milioni saba.

Alisema kwa kuwa kahawa kama inajulikana kote duniani, kitu muhimu sokoni ni ubora ndiyo sababu JJAD imeamua kuzalisha kahawa yenye kukidhi ubora.

Kutokana na hilo, kuanzia msimu 2019/20, bodi ya kahawa ilianzisha mashindano ya ubora wa kahawa kwa wazalishaji wote kutoka sehemu zote nchini ili kuwafanya wakulima kuwa na utamaduni wa kuzalisha kahawa bora.

# Wakulima wapewa mbegu pamba bure

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

ZAIDI ya wakulima 320 wa pamba Kata ya Nyankende, Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamepatiwa kilo 30,000 bure za mbegu ya zao hilo na serikali zenye thamani ya Sh. milioni 49.5 ili kuongeza uzalishaji.

Wakulima hao ni vijana wenye umri wa kuanzia miaka 14 na kuendelea ambao sio wanafunzi na kila mmoja anatakiwa kulima hekari nne za pamba na atakayeshindwa kulima atachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kuondolewa katika kata hiyo.

Akikabidhi pembejeo hizo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alisema, lengo la utoaji wa pembejeo hizo bure ni kuwajengea uwezo wakulima wa pamba na mazao mengine ya kibiashara na msimu ujao Ushetu itakuwa kinara kwa uzalishaji wa zao hilo.

Alisema licha ya kutoa mbegu hizo bure, Wizara ya Kilimo kupitia Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) watatoa dawa na viuatilifu kwa wakulima, hivyo vijana watakaouza mbegu hizo kwa tamaa ya fedha wajiandae kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Kazi hii ya ugawaji wa mbegu bure kwa vijana wa miaka 14 ambao sio wanafunzi na kulima heka nne za zao la pamba ni maagizo ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan na Halmashauri ya Ushetu tumeandikisha vijana 86,000 wote watapata mbegu na watalima pamba," alisema Kiswaga.

Ofisa Kilimo wa Nyankende, Vidisint Mamlima, aliwataka vijana hao kufuata maelekezo ambayo amekuwa akiwapatia mara kwa mara kuhusu namna ya kulima kisasa na kufuata kanuni 10 za kilimo hicho ili kupata pamba safi na yenye ubora, ambao utakubalika sokoni.

Rose Daniel, mmoja wa wakulima kutoka Kijiji cha Mwadui, alisema walikata tamaa ya kuendelea kulima kilimo cha pamba kwa sababu awali walikuwa wakikopeshwa na wakikatwa fedha na vyama vya msingi baada ya mauzo, hali ambayo iliwafanya kushindwa kuendelea kulima.

## Vijana 200 kulipiwa mafunzo kompyuta

**Na Dinna Maningo,** MUSOMA

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ustadi Mkoa wa Mara, inatarajia kuwalipia ada vijana 200 walio na umri chini ya miaka 35 kupata mafunzo ya kompyuta kwa kipindi cha miezi minne yatakayoanza Novemba 18, 2021.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Mkuu wa Chuo cha VETA mkoani humo, Vedasto Lutahakana, alisema mafunzo hayo yanatolewa na serikali kupitia mradi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ili kuwawezesha vijana kupata ufundi stadi na kujitegemea.

Lutahakana alisema kuwa hadi kufikia Novemba 8, 2021 vijana 130 wamechukua fomu ya kujiunga na mafunzo hayo na wengi wanatoka Mkoa wa Mara.

"Ada kwa mwaka kwa fani zote ni 60,000 kwa kila kozi, lakini serikali italipa ada kwa kila kijana, serikali imeamua kuhudumia wananchi wake hasa vijana kupitia vyuo vya ufundi.

Alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajenga vijana stadi za maisha ili wakitokana huko wawe na uwezo wa kujiajiri au kuajiriwa.

"Sifa za kujiunga ni Watanzania wote wenye umri usiozidi miaka 35, ni mafunzo ya miezi minne na miezi miwili mafunzo ya mazoezi kwa vitendo (field) awe na cheti cha kuzaliwa."

Alisema kuwa mafunzo hayo yatasaidia kupunguza mienendo mibovu kwa baadhi ya vijana ambao hawakuwa na kazi za kufanya.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, akiwa amefungwa mguu kwa kutumia nyaya ya umeme na Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Regine Hess ikiwa ni mfano jinsi wanyamapori wanavyonaswa katika mitego ambayo imekuwa ikitegwa na majangili kwa ajili ya kuua wanyamapori na kujipatia kitoweo, katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere. **PICHA: WMU**

# Wizara yaharibu mitego 380 kuulia wanyamapori

**Na Lusungu Helela**

WIZARA ya Maliasili na Utalii imetegua nyaya za umeme 380 zilizokuwa zimetegwa katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ikiwa ni aina mpya ya ujangili dhidi ya wanyamapori kwa ajili ya kitoweo.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, akiwa ameambatana na Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Regine Hess, katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere iliyopo mkoani Morogoro juzi, ameishukuru serikali ya Ujerumani kwa kufadhili mradi huo wa kunasua mitego iliyotegwa kwa ajili ya kuua wanyamapori.

Alisema majangili hao wamekuja na mbinu mpya baada ya serikali kupambana na ujangili wa biashara ya wanyamapori wakubwa kama vile tembo na faru.

Dk. Ndumbaro alisema ujangili wa wanyamapori kwa ajili ya kitoweo kwa kutumia nyaya za umeme, umeanza kuchukua sura mpya huku serikali ikiahidi kuendelea kupambana na mbinu hiyo mpya.

Kwa mujibu wa Dk. Ndumbaro, tangu kikosi maalumu kilichoundwa kwa kushirikiana na wanavijiji kwa ajili ya kutegua mitego hiyo, wanyamapori watatu walikutwa wamekufa baada ya kunaswa kwenye mitego hiyo. Aliwataja wanyamapori waliokutwa wamekufa kuwa ni twiga moja na swala wawili.

Dk. Ndumbaro alisema kupitia mradi huo wa kunasua mitego, wizara imekuja na mbinu ya kuwashirikisha wanavijiji wanaopakana na hifadhi kwa ajili kupambana na majangili hao.

Akizungumzia aina mpya hiyo ya ujangili, Dk. Ndumbaro alisema majangili hao wamekuwa wakitega mitego hiyo kwa ajili ya kuwanasa wanyamapori kwa ajili ya kujipatia nyama ya kula.

Licha ya mitego hiyo kutegwa kwa ajili ya kuua wanyamapori wadogo wadogo kwa ajili ya kitoweo, waziri alisema mitego hiyo inaweza kunasa hata wanyamapori wakubwa kama vile tembo.

Alisema baadhi ya watu katika jamii wamekuwa wakiendeleza imani potofu ya kula nyamapori kwa kuamini kuwa ndiyo nyama bora kupita zote hali ambayo imekuwa ikichangia ujangili kwa ajili ya kitoweo.

Balozi Hess alisema serikali yake iliamua kufadhili mradi wa kutegua mitego hiyo baada ya serikali ya Tanzania kufanikisha kukomesha ujangili kwa asilimia 90 husussan ujangili wa biashara.

Hess alisema mradi huo pia umeonyesha mafanikio makubwa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambapo mitego mingi imeteguliwa.

Balozi huyo aliipongeza serikali ya Tanzania kuwa ya kwanza barani Afrika kwa kusimamia shughuli za uhifadhi kwa ukamilifu.

# Ubovu vifaa vya mawasiliano wapatiwa suluhu

**Na Maulid Mmbaga**

KAMPUNI za Vodacom na Carlcare zimepata suluhisho la changamoto ya kuharibika simu za wateja kwa kuanzisha huduma ya matengenezo katika baadhi ya vituo vyao nchini.

Akizungumza jana Dar es Salaam, mkuu wa kitengo cha mauzo na usambazaji kutoka Vodacom, Deorge Lugata, alisema awali wateja wao walilazimika kushughulikia matengenezo ya vifaa hivyo wenyewe suala ambalo lilikuwa ni adha kubwa kwao.

Alisema kwa Dar es Salaam huduma ya matengenezo kwa wenye uhitaji itatolewa makao makuu na Mlimani City, mikoa mingine ni Morogoro, Ruvuma, Lake Kigoma, Mwanza, Kahama, Geita, Mbeya, Njombe, Arusha na Dodoma.

"Huduma hii itakuwa ni ya uhakika kwani wenzetu Carlcare inayojihusisha na ukarabati wa vifaa vya simu, wana utaalamu na mafundi wao wote wamepatiwa mafunzo kamili nasi tumewawezesha kutekeleza kazi yao hivyo Watanzania waondoe wasiwasi," alisema Lugata.

Mkurugenzi msaidizi wa Carlcare, Winniel Michael, alisema wanashirikiana na zaidi ya kampuni sita za simu kuwafanyia ukarabati wa vifaa vyao huku akiwahakikishia wananchi utoaji wa huduma kwa wakati.

"Dhumuni letu ni kuhakikisha kwamba Watanzania wanaondokana na tatizo la kuharibikiwa na vifaa vyao vya mawasiliano, tuna mafundi wenye weledi na wanatumia vifaa vya kisasa, tumedhamiria kutoa huduma hii kwa manufaa ya wateja na taifa kwa ujumla," alisema Michael.

HABARI KITAIFA

# Marekani yawafundisha wajasiriamali wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI wanawake 32 mkoani Mwanza wamepewa mafunzo maalum ya wiki 13 kwenye biashara na ujasiriamali yaliyofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia programu yake ya kuwajengea uwezo wajasiriamali wanawake (Academy of Women Entrepreneurs -AWE).

Hayo yalibainishwa hivi karibuni wakati wa mahafali yao yaliyohudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, Makamu Mkuu wa Chuo cha Mt. Augustine (SAUT), Serikali ya Marekani iliwakilishwa na Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright na wageni wengine.

Wanawake hao walipongezwa na kuhimizwa kuendelea na kuboresha shughuli zao za uzalishaji mali na kujiongezea kipato.

Akizungumza na wahitimu katika mahafali hayo, Balozi Wright alisema: "Mafunzo ya wiki 13 mliyoyapata mkiwa sehemu ya programu hii yamewapa ujuzi kwa vitendo utakaowawezesha kuanzisha biashara endelevu pamoja na kuwaunganisha na wakufunzi na wajasiriamali kama ninyi wa nchini Marekani."

"Jitihada za wanawake huwa na matokeo makubwa zaidi kwa jamii nzima kwa sababu wanawake wanapofanikiwa mara nyingi watawekeza mapato yao katika familia na jamii zao, wakigharamia mahitaji kama vile ada kwa watoto wao na huduma za afya," alisema Balozi huyo.

Kwa mujibu wa Balozi Wright, manufaa ya kiuchumi ya mafanikio yao yanasaidia vizazi vijavyo na kwamba ubunifu wao unaleta matokeo chanya katika jamii na uchumi wa Tanzania.

Kundi la wahitimu wa Mwanza ni la nne kwa washiriki wa programu hiyo na la kwanza wanawake 20 kuhitimu Septemba 9, 2019 Dar es Salaam, la pili walikuwa 25 kutoka Iringa lilihitimu Desemba 16, 2020 na la tatu washiriki 17 kutoka Zanzibar lilihitimu Juni 28, mwaka huu. Alisema kupitia ubia na Taasisi ya Marekani ya Maendeleo ya Afrika (U.S. African Development Foundation -USADF), wajasiriamali wanaoshiriki programu ya AWE wanaweza kupatiwa fedha za mtaji na USADF Dola za Kimarekani 25,000 ili kupanua biashara zao.

Ubalozi wa Marekani unashirikiana na Selfina kutekeleza programu ya AWE nchini, ikiwa imeanzishwa mwaka 2002 na Dk. Victoria Kisyombe, Selfina ni taasisi ya kitanzania ya utoaji mikopo midogo iliwalenga zaidi wajane na wasichana na kwa miaka 19 wanawake 31,000 wamewezeshwa kiuchumi.

Alisema maisha ya zaidi ya watu 300,000 yamegushwa kutokana na faida zilizopatikana kutokana na mikopo hiyo na kwamba wanamiliki biashara zao wenyewe na zaidi ya nafasi za ajira 150,000 zimetengenezwa.

AWE ni mpango wa kimataifa wa Serikali ya Marekani wa kuwawezesha wanawake kiuchumi unaokusudia kuwajengea uwezo milioni 50 duniani kote kufikia upeo wa uwezo wao kiuchumi.

AWE ina dhamira ya dhati ya kuwapa wanawake elimu na ujuzi, kuwajengea mitandao na kufungua fursa wanazohitaji ili kuyabadilisha mawazo yao kuwa miradi halisi ya kujiletea kipato.

## Stanbic yatajwa ubora uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imetajwa kuwa benki bora ya uwekezaji nchini Tanzania kwa mwaka wa 2021 na EMEA Finance.

Tuzo za EMEA Finance African Banking zinaangazia benki bora zaidi za kibiashara na uwekezaji katika bara zima la Afrika, ikiwa ni pamoja na mawakala na wasimamizi wa amana za uwekezaji.

Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Stanbic Tanzania, Kevin Wingfield, aliwashukuru wateja wa benki hiyo na kusema tuzo hiyo ni matokeo ya juhudi za pamoja kati ya wateja na washirika wengine, akaongeza kuwa vipaumbele vya kimkakati vya benki hiyo ni kukuza ukuaji endelevu na thamani nchini, kwa kutoa huduma za uwekezaji na huduma zingine za benki zinazowezesha miradi muhimu kutekelezwa.

"2021 umekuwa mwaka wa mabadiliko katika sekta ya benki, wakati ambapo uchumi wa dunia ukiendelea kuimarika kutokana na athari za janga linaloendelea la UVIKO-19. Tuzo hii ni uthibitisho wa kina cha utaalamu ambao tunatoa katika huduma za kibenki za uwekezaji nchini na bara la Afrika. Tunawashukuru wateja wetu kwa kutuamini kuwahudumia," alisema Wingfield.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Kitengo cha Uwekezaji wa benki hiyo, Elibariki Ndossi, alisema ushindi wa tuzo hiyo unathibitisha ukakamavu wa benki hiyo katika kukabiliana na changamoto na uongozi bora katika nyanja ya uwekezaji.

"Kwa miaka mingi, tumejenga uwezo dhabiti wa ushauri wa uwekezaji na mikopo ndani ya nchi, na kutoa ufumbuzi kukidhi mahitaji maalum kwa wateja wetu na kutoa huduma nyingi za kibenki za uwekezaji kote nchini," alisema Ndossi.

Benki ya Stanbic imeshirikiana na wateja katika miradi kadhaa ya maendeleo ikiwa ni pamoja na sekta za miundombinu, nishati, mafuta na gesi, viwanda, ujenzi, na miradi ya biashara. Benki inaamini kuwa ufadhili wa maendeleo ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi na ni ufunguo wa kufikia malengo ya Tanzania ya viwanda.

Zaidi ya benki 200 katika bara zima zilishiriki katika tuzo za mwaka huu za EMEA Finance African Banking na Benki ya Stanbic ilishinda katika kitengo cha benki za uwekezaji dhidi ya benki zingine.



Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda (kulia), akimkabidhi mfuko wa mbolea mmoja kati ya wakulima wa Kijiji cha Ugwachanya, Wilaya ya Iringa jana, wakati wa zoezi la kampuni ya One Acre Fund kukopesha pembejeo za kilimo kwa wakulima hao. Nyuma ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (mwenye miwani). **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Wananchi waajiri kampuni kulinda mtaa

**Na Abdul Kingo**

WAKAZI wa Mtaa wa Kichemchem, Kata ya Mbagala Kuu, Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam, wameungana na kuajiri kampuni binafsi ya ulinzi wa eneo lao kwa ajili ya kukabili uhalifu ulioshika kasi hivi karibuni.

Uamuzi huo ulifikiwa kwenye mkutano wa wananchi baada ya Mwenyekiti wa Mtaa, Mussa Magenge, kueleza juu ya kuibuka kwa wimbi la vibaka wanaopora na kuvunja nyakati za usiku.

Wananchi hao walitangaza zabuni kwa kampuni binafsi ya ulinzi kuomba kupewa kazi ya kulinda mtaa huku wananchi wakitakiwa kuchangia gharama kidogo ya ulinzi huo.

Kampuni iliyopitishwa ni ya Wido Security ambayo iliwakilishwa na Salehe Tengeneza, na baada ya majadiliano wananchi walikubaliana kulipa Sh. 1,500 kila kaya kuanzia Desemba, mwaka huu.

Diwani wa Kata ya Mbagala Kuu, Maanya Juma, aliwataka wananchi kuendelea na jitihada hizo za ulinzi kwenye mtaa wao kwa faida yao.

Alisema ofisi imepokea taarifa za kuibuka kwa wimbi la vijana wanaofanya uhalifu usiku kwa kuwapora watu wanapotoka na kurudi kwenye shughuli zao za kujipatia kipato.

# Fursa mpya nafaka Tanzania yapatikana

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Dk. Anselm Moshi, amesema bodi hiyo imeingia makubaliano na kampuni ya Twiga Foods Limited ya Kenya ili kufanya biashara ya pamoja katika soko la Kenya kwenye mazao ya nafaka kama vile mahindi na mchele.

Makubaliano hayo yanafungua ukurasa mpya katika soko la nafaka kati ya Kenya na Tanzania ili kuleta tija kwa wakulima na wazalishaji wa nafaka hasa kwa Tanzania ambao wanazalisha kwa wingi kwa ukanda wa Afrika Mashariki.

Akizungumza na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Twiga Foods Limited ya Kenya, Yabeltal Getachew, Dk. Moshi alisema Bodi ya Mazao Mchanganyiko Tanzania imeendelea kupanua wigo wa masoko kwa kufanya kazi na wafanyabiashara mbalimbali katika ukanda wa Afrika Mashariki ili kujenga soko imara kwa wazalishaji wa mazao ya nafaka nchini.

"Nimefanya ziara hii ya kikazi jijini Nairobi, Kenya katika jitihada za kupanua masoko ya mazao ya wakulima wetu kule Tanzania na lengo la kutembelea kampuni ya Twiga Foods Limited ni kufanya mazungumzo nao na kujenga msingi wa kibiashara kati ya nchi zetu mbili ili wakulima wetu wasihangaike kutafuta masoko ya kuuza mazao yao," alisema.

Aliongeza kuwa wamekwenda Kenya kwa mwaliko wa kampuni hiyo ili kuona miundombinu yao kwa ajili ya kupokea, kuhifadhi na kusambaza nafaka ambazo zinazalishwa na Bodi ya Mazao Mchanganyiko ya Tanzania, ambapo kumekuwa na mazungumzo ya muda mrefu, lakini hatimaye walifikia makubaliano na kutia saini mkataba wa ushirikiano.

Dk. Moshi alifafanua kuwa kampuni hiyo inayo miundombinu ya kisasa ya kupokea, kuhifadhi na kusambaza nafaka, zikiwamo roboti mbalimbali, jambo ambalo limetuvutia kufanya nao kazi wakiamini kutakuwa na ufanisi mkubwa katika ushirikiano huo.

Alisema Tanzania ina uwezo mkubwa wa kuzalisha nafaka na mazao mengine ya mikunde, mtama, mboga, matunda na maua, hivyo akaahidi watafanya nao kazi kwa manufaa ya nchi zote mbili.

"Jambo kubwa ambalo wao wamelieleza ni kumfikishia mlaji chakula kwa bei nafuu zaidi na kwa mtazamo wetu hili ni jambo muhimu sana kwamba mlaji aweze kupata chakula kwa bei nafuu na kiasi kingine cha fedha zake akitumie katika shughuli za maendeleo," alisema.

Dk. Moshi alifafanua kuwa katika nchi za Kiafrika, uzalishaji wa chakula unafanywa na wakulima wadogo, hivyo kuna haja kuwekeza kwa wakulima wadogo ili kuwasaidia kujikwamua kiuchumi kwa kuwaunganisha pamoja katika vikundi au vyama vya ushirika waweze kuzalisha kwa tija na kupata mazao mengi, pia kuuza kwa bei nafuu.

"Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko tutashirikiana na wenzetu ambao tayari wao wanamtandao mkubwa wa masoko ili kuwaunganisha wakulima wetu na kuingia nao mikataba ambayo itawawezesha kuuza mazao yao bila tatizo baada ya kuzalisha," alisema Dk. Moshi.

Makubaliano hayo ni sehemu ya matunda ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoifanya Kenya Mei 6, mwaka huu, ikichangia kwa kiasi kikubwa kufungua milango na kuimarisha uhusiano wa kibiashara kati ya nchi hizo mbili.

Rais Samia alisisitiza umuhimu wa mataifa hayo mawili, Kenya na Tanzania kushirikiana bila kuwapo ushindani, kauli au vitendo vya kukwazana.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Twiga Foods Limited, Yebeltal Getachew, alisema amefurahishwa na ujio wa Mkurugenzi wa Bodi na wako tayari kufanya biashara na bodi hiyo kwa kuwa wana uhakika wa kupata bidhaa kwa wakati na ubora unaohitajika.

"Sisi na Tanzania ni ndugu, mimi mwenyewe nimewahi kuishi Tanzania na tunasambaza baadhi ya chakula kutoka Tanzania, hivyo natazamia kufanya kazi na bodi kwa karibu sana kwa manufaa ya wananchi na nchi zote mbili," alisifu Getachew.



Mwakilishi kutoka Chama cha Ugonjwa wa Kisukari Tanzania (TDA), Dk. Rachel Nungu (kushoto), akitoa maelezo kwa Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Hargeney Chitukulo (kulia), kuhusu wanavyopima watu magonjwa yasiyoambukiza katika wiki ya maadhimisho ya magonjwa hayo kitaifa, mkoani humo. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# TAKUKURU yafuatilia bil. 14/- za madarasa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Morogoro, imeanza kufuatilia Sh. bilioni 14. 1, zilizotolewa na serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 707 kwa halmashauri zilizopo Mkoa wa Morogoro, kwa ajili ya wanafunzi wanaotarajia kujiunga na kidato cha kwanza mwakani.

Mkuu wa TAKUKURU mkoa huo, Manyama Tungaraza, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa umma kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2021.

Alisema Oktoba hadi Desemba 2021, imejiwekea mikakati mbalimbali ikiwa na ufuatiliaji wa fedha hizo zilizotolewa kwa halmashauri zote tisa kulingana na mgawanyo wa mahitaji husika. Pia, alisema kwa serikali kutoa fedha hizo ni muhimu kwa watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia ujenzi wa madarasa, kuhakikisha shilingi ya mwisho inatumika ipasavyo.

Tungaraza alisema hatua kali zitachukuliwa kwa wote, ambao kwa namna moja au nyingine wamejipanga kuzifanyia fedha hizo ubadhirifu fedha hizo zilizotolewa naserikali, kwa ajili ya Watanzania maskini wenye kiu ya kupata huduma bora ya elimu.

Tungaraza aliwataka wananchi kwenye maeneo ya miradi mbalimbali kufuatilia kwa karibu, kulinda vifaa kwa kuwa ni kwa faida yao na serikali imewapunguzia mzigo wa kuchangia ujenzi.

# Wakulima wa korosho wazoa zawadi ushindi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wa korosho mikoa ya Lindi na Mtwara wamekabidhiwa zawadi za aina mbalimbali 26 zenye thamani ya Sh. milioni 20.

Wamepata zawadi hizo kupitia kampeni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani" kutoka Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Zawadi hizo ni baiskeli, pikipiki, pampu za kupulizia dawa mikorosho, guta (Toyo) pamoja na zawadi nyingine ikiwamo kanga, mabegi ya shule na madaftari.

Kampeni hiyo inalenga kusaidia jitihada zilizowekwa na serikali za kuongeza uzalishaji wa korosho kutoka tani 280,000 zinazozalishwa sasa hadi kufikia tani 700,000 ifikapo mwaka 2025 sambamba na kuwahamasisha wakulima wa korosho kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza uzalishaji.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigadia Jenerali Marco Gaguti, alikabidhi zawadi hizo kwa washindi wa kampeni hiyo mkoa wa Mtwara wakati wa mnada wa Chama cha Ushirika cha Masasi, Mtwara na Nanyumbu (MAMCU), uliofanyika katika kijiji cha Njengwa Wilaya ya Mtwara.

"Naishukuru Benki ya NBC kwa kuanzisha jitihada hizi zinazolenga kuunga mkono juhudi za serikali zinazolenga kusaidia wakulima katika kuboresha kilimo cha korosho ili kuongeza uzalishaji wa korosho katika mkoa wetu sambamba na kuboresha maisha yao binafsi na familia zao," alisema Gaguti.

Aliwataka wakulima hao kutumia vifaa hivyo ipasavyo ili viweze kuwasaidia katika kuhakikisha wanaongeza uzalishaji wa zao hili kwa kujiandaa vema kwa ajili ya msimu ujao.

Akikabidhi zawadi hizo upande wa mkoa wa Lindi, Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, aliwataka wakulima wa korosho mkoani humo kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza ili kuboresha uzalishaji wa mazao yao na kujikwamua kiuchumi.

"Pamoja na kuwapongeza washindi wa droo hii nawaomba sana wazitunze zawadi zao ili ziweze kuwasaidia katika shughuli za kilimo cha korosho kama ilivyokusudiwa...na zaidi nawapongeza Benki ya NBC kwa kuona umuhimu wa kutoa zawadi zinazoendana na aina ya kilimo husika," alisema Ndemanga.

Mkuu wa Bidhaa na Mauzo wa Benki ya NBC, Abel Kaseko, alisema kampeni hiyo inalenga kuwahamasisha wakulima wa zao la korosho katika mikoa ya Lindi na Mtwara ili waweze kujikwamua kutoka kwenye changamoto mbalimbali za huduma za kifedha zinazokwamisha jitihada zao za kujikwamua na umaskini kupitia kilimo cha zao hilo.

"Naendelea kuwahamasisha wakulima waendelee kupitishia fedha zao kupitia benki akaunti ya NBC Shambani ili wawe kwenye nafasi ya kujishindia zawadi lukuki katika droo zinazofuata," alisema Kaseko.

ama
ALHAMISI NOVEMBA 11, 2021
AFYA NA MAZINGIRA


Ukurasa 12

**Mikasa, mateso yanayowakuta watoto wenye vichwa vikubwa na wazazi wao**


Ukurasa 13

Mabingwa Muhimbili wafukua kilichomo katika masamiati ugumba, madhara yake


Ukurasa 14

**Watafiti TALIRI Mwanza waibua majani kupandikiza kumaliza mgogoro malisho**

# Kuhamia mbegu chotara ilivyombadili mfuga ng'ombe ghafla 'mifuko kutuna'

**Neema Emmanuel na Lilian Lugakingire,** MWANZA


Mtafiti wa Mifugo kutoka kituo cha TALIRI Mwabuki, Godfrey Chasame, akimpa maelekezo ya namna ya uangalizi wa ndama mtoto wa mfugaji, James Manjala. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

Ni maajabu ya teknolojia, ng'ombe mmoja kuwa kiungo cha ongezeko wakatimu zaidi ya 50 na ndama zaidi ya 47. Hiyo ni ndani ya kipindi cha miaka minne na kuboresha maisha ya mfugaji.

James Manjala, ni mtoto wa mfugaji anayesimulia namna ng'ombe mmoja dume aina ya Ankole, ilivyoleta mwanga na tabasamu katika familia yao kiuchumi, hata maendeleo yakashuhudiwa watoto kupata elimu bora kupitia mifugo hiyo.

Manjala ambaye pia yuko masomoni katika ya taaluma ya mifugo, anaeleza namna walianza na teknolojia hiyo ya uboreshaji wa ufugaji wa ng'ombe wa asili kwa kutumia dume aina ya Ankole mara baada ya kupewa elimu ya kutosha na kituo cha utafiti wa Mifugo(TALIRI)- Mabuki. Baada ya hapo, wakafanya uamuzi kulichukua dume hilo ambalo limewaletea mabadiliko katika maisha.

Anasema awali kabla hawajaanza kutumia teknolojia hiyo, walikuwa na ng'ombe 100 hadi mwaka 2017 walipoingia rasmi katika kutumia mfumo huo na mifugo ikaongezeka hadi wakafika jumla 150.

Faida ilianza kuonekana na kukidhi mahitaji yao ikiwamo kusomesha wanafunzi, kununua viwanja na kuboresha maisha, tofauti na ilivyokuwa awali.

"Kuanzia mwaka 2017 siyo kwamba tumeongeza ng'ombe hao tu 50 ni wengi sana, lakini ilitulazimu kuwapunguza kuweza kumudu malisho ambayo yanapatikana kwa umbali mrefu na kwa shida. Pia, wakati mwingine yanajitokeza magonjwa, lakini tunawatibu na kupona," anaieleza

Kuhusu soko la bidhaa yao, anasema walipowauza ng'ombe wa kienyeji walipata fedha kidogo, ng'ombe mwenye umri miaka miwili walimuuza kwa Sh.100, 000 hadi Sh. 200,000.

Anasema, kwa sasa hali ni tofauti wanapata faida kubwa kulingana na ukubwa na ubora wa mfugo huo ambao wa miaka hiyo wanauza kwa bei kuanzia Sh. 900,000 hadi Sh. million 1.5.

Pia, anarejea zama hizo walipohitaji fedha wastani Sh. milion moja walilazimika kuuza ng'ombe kuanzia watatu na sasa wanauza mmoja pekee.

Anausifu mchanganyiko huo wa ng'ombe aina ya Ankole na wa kienyeji wanakua haraka, wa umri mwaka mmoja analigana na aliye na miaka miwili, hata gulioni anawasifu wanakubalika zaidi kwa wateja.

Pia, katika utoaji maziwa anawasifu wako juu, kwani inapatikana lita moja na nusu hadi mbili, kutoka robo za awali.

"Japokuwa mimi ni mtoto wa mfugaji, niliwapenda sana mifugo, hivyo nikaamua kwenda kusomea kozi ya mifugo na sasa nipo ngazi ya diploma ninasomeshwa na baba kupitia ng'ombe hawa. Mie natarajia kuwa mfugaji bora wa kisasa," anaeleza Manjala

Kaimu Mkurugenzi wa TALIRI Kanda ya Ziwa kituo cha Mabuki Dk. Heriel Massawe, anaeleza kuwa mwitikio wa wafugaji kutumia teknolojia hiyo umeongezeka, pia kuna ufasaha kwenye maeneo mengi.

Anayataja kuwa ni katika kusambaza madume bora ya ng;ombe, kutolewa elimu ya ufugaji bora na kufuatilia matunzo na ukuaji bora wa ndama chotara.

Dk. Massawe anafafanua kuwa, kuna madume 40 bora ya Ankole na Mpwapwa, yaliyosambazwa kwa kuwauzia wafugaji katika wilayani za Misungwi, Kwimba, Magu, Itirima na Bunda.

Hadi sasa kuna ndama chotara 400 waliozaliwa na mwitikio wa wafugaji, wameona matokeo mazuri na yenye faida kwa kutumia mfumohuo.

Mtafiti Mifugo kutoka kituo cha TALIRI, Mwabuki Godfrey Chasamu, anasema wamejikita zaidi kwenye ng'ombe wa nyama, kwa sababu ndio wametawala katika Kanda ya Ziwa.

"Wafugaji ni watu muhimu kwa sababu wao ndio wanazalisha nyama inayoingia sokoni na kutulisha watu wote," anasema Chasamu,

Aidha, Mkurugenzi wa Menejimenti ya Maarifa kutoka Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) Dk. Philbert Luhunga, ana ufafanuzi kuwa serikali imewekeza fursa kubwa kwenye taasisi za utafiti zikitoa matokeo ya kisayansi na kuzilekeza katika jamii, hasa katika tafsiri ya kuhudumia wananchi wa ngazi ya chini.

Hivyo, teknolojia za ng'ombe wa kisasa wanaotoa nyama nyingi na kukua kwa muda mfupi, ina manufaa maradufu kwa umma husika, mfano hao ni pale ng'ombe wao zamani aliuzika kwa wastani wa Sh. 300,000 na sasa ng'ombe huyo ana bei mpya inayogota kuanzia Sh. 700,000 hadi Sh. milioni moja.

*Soma zaidi Uk. 14*

AFYA

# Mikasa, mateso yanayowakuta watoto wenye vichwa vikubwa na wazazi wao

• Bingwa Dk. Ngiloi: Inazuilika, serikali ikifanya hivi...

**Na Dk. Ananilea Nkya**

FAMILIA nyingi nchini zenye watoto waliozaliwa na kichwa kikubwa (hydrocephalus) zinateseka kutokana na kunyanyapaliwa, pia kufiwa na watoto kwa kukosa fedha za kuwatibu, ingawa ni ulemavu unaozuilika.

Daktari bingwa wa upasuaji watoto, Petronilla Ngiloi, anasema chanzo kikubwa cha mtoto kuzaliwa na kichwa vikubwa ni mama kubeba ujauzito wakati mwili hauna madini ya folic acid.

Anasema kuzuia mtoto asizaliwe akiwa na kichwa kikubwa, mama anapaswa kabla ya kubeba ujauzito awe amekula vyakula vyenye virutubisho vya madini hayo, angalau miezi sita mfululizo na aendelee kula wakati wote wa ujauzito na baada ya kujifungua.

Daktari huyo anasema, wanawake wenye umri wa kubeba mimba na Watanzania wote wanaweza kuondokana na ukosefu wa madini hayo mwilini, kama serikali itachukua hatua kuweka madini hayo kwenye mlo unaotumiwa na wengi, mfano chumvi.

Anasema inawezekana, kwa sababu huko nyuma serikali ilishachukua hatua kama hiyo kuweka madini ya iodine kwenye chumvi kuzuia umma usipate ugonjwa wa tezi la shingo (Goita).

"Kwa sababu watoto wengi wanaozaliwa na kichwa kikubwa ni wale wa familia ambazo hazina uwezo," anasisitiza bingwa huyo wa tiba magonjwa ya watoto wadogo.

Dk. Ngiloi anatoa mfano nchini Uholanzi walikofanikiwa kudhibiti watoto kuzaliwa na ulemavu huo, baada ya serikali kuamua kuweka madini 'folic acid' kwenye mlo wao unaotumiwa na wengi 'cheese.'

Hadi sasa, Tanzania imo katika nchi za Afrika Kusini mwa Janga la Sahara zinazosumbuliwa na tatizo la watoto kuzaliwa na ulemavu wa kichwa kikubwa na taarifa za kimtandao zinabainisha ukanda huo unapata watoto aina hiyo 100,000 kila mwaka.

Daktari Ngiloi, anasema Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), hupokea watoto kati ya 300 na 400 kwa mwaka wenye tatizo hilo.

## GHARAMA KUBWA

Dk. Ngiloi anasema mtoto anayezaliwa na ulemavu wa kichwa kikubwa, huhitaji matibabu ya upasuaji aweze kuwekewa mrija maalum unaojulikana kitaalamu kama "ventriculoperitoneal shunt (VPS)" wenye uwezo wa kuondoa maji kichwani kila wakati na kumuwezesha kuishi.

Anasema kabla ya kufanyiwa upasuaji, wanaanza na kipimo cha 'X-ray' kufahamu undani wa tatizo. Dk. Ngiloi anafafanua: "Matibabu haya ni ya gharama kubwa, yanaweza kufikia Sh. milioni moja na zaidi."



Daktari Bingwa Mshauri Mwelekezi wa Upasuaji wa Watoto, Petronila Ngiloi (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, hawapo pichani. **PICHA: MTANDAO**

> **Baada kutumia dawa, kidonda kilipona isipokuwa walilazimika kurudi tena hospitali, maana kichwa cha mtoto kilianza kuvimba na kinachobonyea.**

## JICHO KWENYE MKASA

Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali linalojishughulisha na lishe bora kwa watoto wenye ulemavu (NPCD) Kanda ya Ziwa, Millicent Lema- Lasway, anasema wamebaini familia zenye watoto wenye ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi (spinalbifida) zinashindwa kumudu gharama za matibabu, hata kusababisha vifo vya watoto wao.

Millicent anatoa ufafanuzi wa watoto wawili kutoka Kanda ya Ziwa, Ayub (mwaka mmoja) na Bhoke (11), ambao NPCD iliwasaidia baada ya familia kukwama fedha za matibabu na wamefariki dunia kwa saabu hawakupata tiba kwa wakati.

Baba mzazi wa Ayub. Japheti Bwegamo wa Kijiji cha Kisanghwe, Kata ya Butundwe mkoani Geita, anaiambia Nipashe kwa njia ya simu kwamba mwanawe alizaliwa Desemba 27 mwaka 2019, katika zahanati ya kijiji hicho alikogundulika na kidonda mgongoni.

Kwa mujibu wa Dk. Ngiloi, mtoto anapozaliwa na kidonda mgongoni(spinalbifida) ni dalili kwamba ana tatizo la kichwa kikubwa.

Bwegamo anafafanua kwamba baada ya kugundulika na hilo tatizo, aliwapatiwa rufani kwenda hospitali ya wilaya ambako nako akapewa rufani kwenda Hospitali ya Mkoa Mwanza,

"Baada ya kupokewa hospitalini, kesho yake mtoto alipimwa kichwa tukalipa elfu thelathini, vipimo na elfu thelathini za dawa ya kupaka kwenye kidonda, kasha," anaeleza, pia akiwa na ufafanuzi wa malipo ya mtoto kukaa hospitalini hapo kwa siku tano.

Anasema baada kutumia dawa, kidonda kilipona isipokuwa walilazimika kurudi tena hospitali, maana kichwa cha mtoto kilianza kuvimba na kinachobonyea.

Baba huyo anasimulia mtoto wake (Ayubu) alifanyiwa upasuaji Januari 25, mwaka jana, kwa malipo ya Sh. 300,000 za vipimo, upasuaji na kumuwekea mrija kutoa maji kichwani.

Mzazi huyo anasema, baada ya mtoto kupata nafuu, miezi kadhaa tatizo lilirejea, maana mirija aliyowekewa kutoa maji kichwani iliziba hata kabla ya siku aliyopangiwa kurejea hospitalini kwa uangalizi, Agosti 31, mwaka jana

Anasema akiwa na mkewe walipompeleka hospitalini walitakiwa kulipa Sh. 300,000 za kufanyiwa upasuaji wa pili, kuwekewa mrija mwingine.

"Hali yetu kifedha ilikuwa mbaya, maana tuliondoka nyumbani na laki moja, elfu arobanini tukawa tumetumia nauli watu wawili mimi na mke wangu na tulikuwa tumebakiwa na elfu sitini tu tukakataliwa tukaambiwa tulipe angalau Sh.150, 000," anaeleza Bwegeno.

Anasema kutokana na kukosa fedha, mtoto hakupata matibabu na walirudi nyumbani kijijini, mtoto akiendelea kuwa na hali mbaya.

Bwegeno, anasimulia kwamba wakiwa nyumbani, walipokea simu kutoka hospitalini Bugando ambako NPCD waliwaaka wafike huko mgonjwa wahudhurie semina wakiwa na mtoto wao.

"Tuliwaambia hatuna uwezo wa kuja hatuna nauli. Waliniomba nitafute nauli angalau mama aende akiwa na mtoto, NPCD itamrejeshea," anaeleza Bwegeno

Anafafanua mkewe alienda na alipofika huko, mtoto huyo alikuwa na hali mbaya na ndipo NPCD ikaamua ichangishe fedha za kumgharamia mtoto vipimo, upasuaji, kuwekewa mrija mpya na gharama za kukaa hospitali siku tano.

Hata hivyo, Bwegemo anasema walipata huduma na baada ya kufika nyumbani, kidonda cha upasuaji hakikuopona na hali ya mtoto iliendelea kuwa mbaya na kwa vile hali yao kifedha ilikuwa mbaya, walishindwa kumrudisha hospitalini na mtoto alifariki Novemba 9, mwaka jana, ikimaanisha leo inatimu mwaka mmoja na siku mbili.

## MZAZI MWINGINE

Baba wa Bhoke, Zablon Maitari, anasimulia Nipashe kwa njia ya simu mkasa wake kutoka kijijini Nyamakobiti, kata ya Majimoto, wilayani Serengeti, mkoa Mara kwamba yeye na mkewe wameteseka sana kumhudumia mtoto wao.

"Tatizo la Bhoke lilikuwa kubwa. Alikuwa na kichwa kikubwa na mgongo wazi...mgongo ulikuwa na shimo, palitoa maji kila wakati.

"Kulikuwa hakuna mawasiliano kutoka kiunoni hadi miguuni kwa mtoto. Alihitaji matibabu na uangalizi wa karibu wakati wote," anaeleza Matairi

Anasema mtoto wake alifanyiwa upasuaji na kuwekewa mrija (shunt) akiwa na miaka mitatu lakini akiwa na umri wa miaka tisa iliziba akafanyiwa upasuaji kuwekewa mwingine.

"NPCD ndio walitutafutia pesa kulipia vipimo, kumfanyia mtoto upasuaji na gharama za kukaa hospitali siku mbili siku ya tatu tukaondoka kwenda nyumbani," anasema Maitari

Anafafanua mtoto wake aliporudi nyumbani, hali yake ilikuwa mbaya zaidi, maana mrija (shunt) aliyowekewa iligoma kufanya kazi na ndani ya wiki tatu walimrudisha hospitalini.

Mzazi huyo anasema, alikaa hospitalini wiki nzima akihudumiwa, akigusia la kipekee: "Alikuwa na maumivu makali sana, kila siku alilia 'ninakufa' 'ninakufa' na akafa tarehe thelathini, mwezi wa nne 2021."

Mama wa Bhoke, Mkwami Matiko, anaendeleza simulizi akimsifu mumewe katika miaka yote 11 ya Bhoke, alijitoa kikamilifu kumlea mwanawe, kinyume na baadhi ya wanaume wanaonyanyapaa familia, penye mikasa ya ulemavu kama huo,

"Hata Bhoke alipokufa, mume wangu ndiye alikuwa naye hospitali, maana mimi nilikuwa mjamzito," anasimulia

INAENDELEA UK.13

AFYA

# Mabingwa Muhimbili wafukua kilichomo katika masamiati ugumba, madhara yake

**Na Christina Mwakangale**

## • Kituo cha Upadikizaji chaja, wataalamu wanolewa



Wajawazito wakipata huduma wodini. **PICHA: MATANDAO**

UNAPOTAJA ugumba, imo katika tatizo linalozikumba jamii nyingi hata kufikia hatua mgogoro na kukatiza uhusiano wao.

Matarajio ya familia nyingi hasa wanandoa, ni kupata watoto muda mfupi baada ya kuonekana ukweli kwamba jambo hilo ni la kibaolojia, imani na lenye kuhitaji subira.

Kitaalamu ugumba unatamkwa kuwa hali ya mwanamke kushindwa kupata ujauzito zaidi ya mwaka mmoja bila ya kutumia njia za kinga za uzazi au mpango wowote. Ni tatizo linalotajwa kuwakumba wenye umri miaka kuanzia 21 hadi 45.

Wanasaikolojia wana maoni dhidi ya dhana potofu kwamba mwanamke pekee ndio chanzo cha kasoro hiyo, ingawa ukweli unamgusa hata mwanamume anayetoa mbegu za uzazi.

### MADAKTARI BINGWA

Bingwa wa Magonjwa ya Kinamama na Uzazi kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Living Colman, anaiambia Nipashe kwamba tatizo hilo linaongezeka nchini na kati ya wagonjwa 10 anaowaona kwa siku, watatu wana tatizo hilo.

"Kesi za 'infertility' ni nyingi sana. Katika kila wagonjwa 10 unaweza kuona watatu au zaidi wenye 'infertility'. Athari za ugumba hasa ni unyanyapaa kwa wanandoa hasa mwanamke.

"Hali inayoweza kupelekea hata ndoa kuvunjika na kuharibu uhusiano wa jamii kwa pande zote mbili, mume na mke," anasema bingwa huyo.

Dk. Colman anasema: "Si kweli kwamba matumizi ya dawa za uzazi wa mpango ndio chanzo cha ugumba. Ikiwa zitatumika kwa maelekezo ya mtaalamu, basi husaidia kuzuia mimba kwa muda fulani na pindi unapoziacha, mama anaweza kuendelea kupata ujauzito kama kawaida.

"Kuwapa watoto dawa za uzazi wa mpango ni kuwapa uhuru wa kufanya ngono zembe, hali inayosababisha kupata maambukizi kwenye njia ya uzazi (PID). Hivyo, kuathiri mirija ya uzazi kushindwa kupata ujauzito mbele."

Dk. Colman anasema ipo haja ya watoto husussan wasichana, kufundishwa kuepuka ngono za mapema zinazochangia maambukizi kwenye mfumo wake wa uzazi na matokeo yake mirija inaziba na kushindwa kushika mimba wakiwa watu wazima, wanapohitaji kuunda familia.

Ili familia iepuke hali hiyo, anasema kuna wajibu wa kutafuta ushauri wa wataalamu wa afya ya kinamama kuhusu afya ya uzazi namna ya kuepuka maambukizi kwenye njia za uzazi, ambayo mirija ya uzazi inaweza kuziba.

### SABABU NINI?

Dk. Colman anasema ugumba una vyanzo tofauti na kwamba kwa mwanamke chanzo kikuu ni mayai kushindwa kupevuka kwa mpangilio (hormonal imbalance), ambayo inatokana na hali ya kurithi.

Kadhalika, Dk Colman anasema ulaji vyakula vingi vya sukari na mafuta, unachangia kuwapo unene uliopitiliza na kupungua uzito unaweza kuwa chanzo ugumba.

"Mirija kuziba ndio sababu ya pili ya ugumba kwa mwanamke na hii husababishwa na ngono zembe," anasema.

Kwake mwanamume, sababu ya ugumba inachangiwa na kushindwa kuzalisha mbegu kutokana na mambo kama ulevi wa kupindukia, pia sigara.

"Pia, sababu nyingine ni kuziba mirija ya kupitisha mbegu inayosababishwa na maambukizi," anafafanua.

### TIBA IKOJE?

Dk. Colman anashauri ni vyema kuwaona wataalamu wa afya ambao hufanya vipimo na kugundua tatizo, kisha wanatoa tiba husika.

"Kama ni 'hormonal imbalance' atapewa dawa na ushauri na iwapo ni mirija imeziba atashauriwa apandikize'.

"Infertility ipo siku nyingi pengine tangu kuumbwa kwa dunia. Hata kwenye vitabu vya dini tunaona jinsi Nabii Ibrahim na Mkewe Sara walikaa muda mrefu bila ya kupata mtoto. Hata Yohana mbatizaji alipatikana baada ya muujiza.

"Kesi za ugumba ni nyingi sana, Katika kila wagonjwa 10 unaweza kuona watatu au zaidi wenye 'infertility'. Hakuna jamii ambayo ipo salama na wote wenye uwezo na wasio na uwezo tatizo lipo. umri ni kuanzia miaka 21 mpaka 45," anasema Dk. Colman.

### UZAZI MPANGO

Katika hoja ya dawa za uzazi wa mpango kati ya sababu za tatizo hilo, Dk. Colman anasema si sahihi kwa kuwa matumizi dawa ya uzazi pasipo kuwapo mpangilo mzuri wa watoto katika familia, ingawa anakiri kuwapo matumizi ya dawa isivyo sahihi.

"Ukitizama kwenye jamii hasa mijini, wengi wanatumia njia uzazi wa mpango wa dharura, njia ambayo si sahihi sana, kwani ikitumika kila mara napoteza maana yake.

"Njia nyingine ni kitanzi na kijiti. Hizi ni za muda mrefu na haziingiliani na mfumo wa maisha wa mtu, yaani akishaweka anaendelea na shughuli zake kama kawaida.

'Kwa uchache watu wanatumia vidonge vya majira na hii ni kwa sababu ya ile hali ya utumwa. Kila siku lazima unywe dawa, inayofanya wengi kuchoka au kusahau na ukisahau kunywa siku moja tu, basi umeharibu dozi nzima," anafafanua bingwa huyo

### KUPANDIKIZA MIMBA

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi kutoka MNH, Nathanael Mtinangi, anasema mahitaji ya upandikizaji mimba(In Vitro Fertilisation – IVF) yanaongezeka kila siku nchini, huku hospitali hiyo ikiandaa kituo cha kibingwa cha upandikizaji ikiwamo huduma ya IVF.

Bingwa huyo anasema, hadi sasa wataalamu wake waliopelekwa na MNH masomoni nje ya nchi, walitarajiwa kurejea mwezi uliopita, jengo mashsusi la mradi linaendelea kujengwa na vifaa kuwekwa.

Anasema huduma hiyo itakapoanza nchini, gharama itakuwa nafuu ikilinganishwa na ilivyo sasa. Gharama nje ya nchi ni kati ya Sh. Milioni 15 hadi 40, kutegemea na aina ya huduma, pia tatizo.

### MWANASAIKOLOJIA

Mtaalamu wa Saikolojia Tiba, Saldin Kimangale, anasema kwenye jamii watoto wana kinga na usalama kwa ndoa na uhusiano na bila ya wao, wanawake hujihisi hawako salama katika uhusiano.

"Kila mwanamke ana njia zake za kujenga maana juu ya tatizo la ugumba. Wako ambao litawasumbua sana na wako ambao litawasumbua kiasi na wako ambao kwao sio tatizo. Hiyo inategemea rasilimali za ndani alizonazo kiwemo ujasiri, kujiamini, uvumilivu, subira, imani.

"Watoto huwa ni kinga na usalama wa ndoa na mahusiano, bila watoto wanawake hujihisi hawako salama katika uhusiano, anasema.

## Mikasa, mateso yanayowakuta watoto wenye vichwa vikubwa, wazazi

**INATOKA UK.12**

### ANGALIZO LA WADAU

Wadau asasi ya NPCD, inaeleza kuguswa na kifo cha Bhoke katika imani huenda uhai wake ungedumu, iwapo angepatiwa matibabu ya ziada na uangalizi wa karibu wa kitabibu hadi kupona majeraha na kuhakikisha mrija mpya aliyowekewa, umekubalika vyema mwilini.

"Ninaamini mikiki ya kusafiri siku ya tatu baada ya upasuaji tena umbali mrefu kwenye mabasi kutoka Mwanza hadi vijijini mkoani Mara inawezekana kulikuwa na athari mbaya kwa mtoto" anasema Millicent, Mkurugenzi wa NPCD.

Ikirejewa Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2017, inalenga kukabili magumu ya afya yanayowakabili wananchi maskini, hasa kuhusiana na kupata fedha za huduma ya afya.

Hapo ndipo penye angalizo la Dk. Ngiloi, akitaka kuwapo mfuko maalumu wa matibabu ya watoto wanaozaliwa na ulemavu kichwa kikubwa, ili wapatiwe tiba kamili hadi kuruhusia kuondoka hospitalini.

Bingwa huyo anasema, watoto wanaozaliwa na vichwa vikubwa wakipatiwa bima za bure na kukawepo na fungu maalum la fedha kuilipia, watakuwa na uhakika wa tiba; kupimwa, kufanyiwa upasuaji na kulazwa hospitalini.

Ni ushauri unaoungwa mkono na Mwenyekiti wa kijiji cha Kasanghwa, Tiro Wakayeye Wasigara, wanakopatikana wazazi wa marehemu mtoto Bhoke.

Wasigara anasema, watoto wenye ulemavu pia wanahitaji kusaidiwa pia huduma nyingine kama baiskeli wamudu maisha yao, akitoa mfano wa kuwapo mtoto kijijini anayeteseka na madhila hayo.

MAZINGIRA

# Watafiti TALIRI Mwanza waibua majani kupandikiza kumaliza mgogoro malisho

- Yaliibiwa nchini zama 1800, yarejeshwa
- Mifugo kushiba, unene na maziwa kibao

**Lilian Lugakingira na Neema Emmanuel**, MWANZA

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) Kituo cha Mabuki iliyoko mkoani Mwanza, inaendesha utafiti wa kuotesha majani ya mifugo hususan ng'ombe, ili kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji, inayotokana na uhaba wa malisho.

Patrick Rukiko, mtafiti wa malisho kituoni hapo, anasema itawezesha kupatikana chakula cha kutosha cha mifugo na kupunguza migogoro, huku ikitoa mazao bora ya mifugo; maziwa na nyama.

Ni hali inayowaongezea pato wafugaji na jamii, huku akitaja wastani asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo na mifugo.

Rukiko anasema sekta ya mifugo pekee inachangia asilimia 7.4 ya Pato la Taifa, ingawa bado mifugo nchini inakabiliwa na shida mbalimbali zikiwamo magonjwa kukosa mbegu bora ya mifugo, maji, maeneo ya kuchunga na malisho.

"Tatizo kubwa ni malisho. Kwa hiyo TALIRI imepata ufadhili kutoka shirika la maendeleo la nchini Sweden (SIDA) kupitia Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI) iliyoko Nairobi nchini Kenya. Tunaendelea kutafuta ufumbuzi wa namna gani tunaweza kutatua tatizo la ukosefu wa malisho," anasema.

Mtafiti huyo anataja aina ya majani Brachiaria yanayotumika katika nchi za Brazil, Australia na Marekani, yameonyesha matokeo bora katika uzalishaji mifugo na ndiyo yanayoendelea kutafitiwa, lengo ni kukabiliana na uhaba malisho kitaifa.

"Haya majani ya Brachiaria inasemekana asili yake ni Tanzania na Congo (DRC na Congo Brazavile) ambayo yalichukuliwa miaka kuanzia 1800 hadi 1900 na kupelekwa katika nchi hizo na kuanza kuyazalisha.

"Baadaye yameletwa tena huku, lakini mbegu yake tunauziwa kwa gharama kubwa ambayo ni kati ya dola 45 hadi 50, kiasi ambacho ni kama Sh.100,000 kwa kilo moja," anaeleza.

**UTAFITI UNAVYOFANYIKA**

Utafiti ulioendelea unaonyesha majani aina Brachiaria yanastahimili misukosuko ya hali ya hewa, yanaongeza uzalishaji maziwa kati ya asilimia 15 hadi 40 na yanaondoa hewa chafu ukaa, pia kurutubisha udongo.

"TALIRI Mabuki na TALIRI Tanga kwa kushirikiana na ILRI ya Nairobi nchini Kenya, tulikusanya sampuli 285 nchi nzima kwa lengo la kutaka kujua kwamba haya majani aina ya Brachiaria yapo ya aina ngapi, maana yanaweza kuwa yanatofautiana kwa kuyaona, lakini ndani hayana tofauti," anaeleza Rukiko.

Anasema baadae walipata sampuli 10 zilizofanya vizuri nchi nzima, tano kutoka TALIRI Mabuki. Pia, anasema walipima vinasaba (DNA) vya majani hayo kudadisi kama ya ukoo mmoja, yakijaribiwa kutoka ikolojia (Mfumo wa maisha na maumbile) nne nchini kujua tofauti zake.

Mtafiti Rukiko anasema majaribio sasa yapo katika kanda nne: Ziwa iliko TALIRI Mabuki; Kati - Mpwapwa; Mashariki, Tanga; na Nyanda za Juu Kusini, Uyole Mbeya.

"Lengo ni kutaka kujua aina hizo kumi kama zinaweza kufanya kazi katika vituo vingine. Baada ya hapo tutaangalia ni mbegu gani imefanya vizuri zaidi katika ukanda fulani au ipi inafanya vizuri katika kanda zote," anafafanua.

Anataja hatua inayofuata, TALIRI inalaenga kujitosheleza kupitia uzalishaji mbegu nchini na kuepuka uagizaji nje ya nchi kwa gharama kubwa.

"Ili tuweze kwenda hatua nyingine mpaka tujiridhishe kuwa hatua ya awali imefanikiwa," anaweka angalizo baada ya kama mwaka mmoja na nusu kuanzia sasa, matokeo yatakuwa yamepelekwa kwa wakulima na wafugaji na kushuhudiwa uzalishaji chakula cha kutosha cha mifugo.

**MADUME NG'OMBE**

Katika maziwa na nyama, anasema TALIRI Mabuki wanaendelea na mradi wa kuboresha uwezo wa ng'ombe wa asili kwa kutumia mbegu aina Ankole kutoka mkoani Kagera.

Godfrey Chasama, Mtafiti Mifugo kutoka TALIRI Mabuki, anasema asilimia 98 ya ng'ombe ni aina ya Zebu, ambao uzalishaji wake sio mzuri kulinganisha na Ankole.

Anasema kinachofanyika ni kuchukua madume Ankole yanapandishwa kwa jike Zebu, kupatikane ng'ombe bora, mradi ulioanzishwa mwaka 2012.

Chasama anasema ng'ombe aina Zebu wana uzito kati ya kilo 300 hadi 350, huku Ankole uzito wao ni kati ya kilo 400 hadi 450 na ladha ya nyama Ankole inaizidi Zebu.

Chasama anataja matarajio ni kutumika teknolojia mbadala ya upandishaji kwa chupa, ili dume liweze kuhudumia ng'ombe wengi na hadi sasa madume yaliyozalishwa kwa mbegu Ankole, hata kusambazwa kwa wafugaji 40, wafugaji wameshaelimishwa na wameanza kuzalisha madume bora kukiwapo ndama 400 hadi sasa.

Mtaalamu huyo anasema dume moja lina uwezo wa kuhudumia ng'ombe majike kati ya 40 hadi 50, lakini dume hilo halipaswi kukaa sana. Ikionekana mitamba iliyozalishwa inakaribia kupandwa, linahamishwa kuepuka lisipandishwe kwa watoto wake.

"Wafugaji tuliowafundisha kutumia teknolojia hii kuzalisha mbegu bora kwa kutumia madume ya Ankole, tunawatembelea kila mara na kuwakagua kuona kama wanazalisha mbegu bora kama ilivyokusudiwa," anaeleza.

Mtaalamu anaendelea: "Hata kama ubora wa mbegu hizo utakuwa haufikii zinazozalishwa na taasisi, lakini lazima tujiridhishe."

"Madume tunayozalisha ni bora maana yanapimwa kasi ya ukuaji wake baada ya kuachishwa kunyonya na baada ya hapo tunachagua ambayo ni bora na yanayoonekana siyo bora yanahasiwa, ili kuzuia kuendeleza kizazi cha mbegu isiyo bora," anasema.

**MKURUGENZI TALIRI**

Kaimu Mkurugenzi wa TALIRI Mabuki, Dk. Hezekiel Massawe, anasema ili kuhakikisha wanatoa huduma bora waliomba fedha Sh. milioni 300 kutoka Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa ajili ya kujenga nyumba tatu za watumishi na maabara ya nyama.

"Nyumba zimekwishaanza kutumika, lakini maabara bado haijaanza kutumika, kwa sababu hatujapata vifaa. Tumeomba tena COSTECH watufadhili vifaa ili maabara hiyo ianze kazi ya kupima nyama, lengo likiwa kupata ubora wa nyama inayozalishwa na sasa tunasubiri mrejesho," anasema.

Dk. Massawe anasema Kanda ya Ziwa ina viwanda vingi vinavyozalisha nyama, hivyo kuna umuhimu wa maabara za kusaidia wanunuzi wa nje ya nchi kujua ubora wa nyama ya nchini ili wajitokeze kwa wingi.

Ripoti ya Mpango Kabambe wa Mifugo Nchini ya Mwaka 2017/2018 hadi 2021/2022, Tanzania inataka mifugo nchini kuna mifugo milioni 30.5 na nchi ya pili Afrika kuwa na mifugo mingi, ikitanguliwa na Ethiopia.



Majani bora na kisasa yaliyooteshwa na TALIRI Mabuki, mkoani Mwanza kwa ajili ya utafiti wa malisho. **PICHA : LILIAN LUGAKINGIRA**

> **"Baadaye yameletwa tena huku, lakini mbegu yake tunauziwa kwa gharama kubwa ambayo ni kati ya dola 45 hadi 50, kiasi ambacho ni kama Sh.100,000 kwa kilo moja.**



## HABARI DODOMA

## Serikali yaanzisha huduma ya kusafisha damu hospitali mikoani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeendelea kusogeza huduma za kibingwa na kibobezi karibu na wananchi kwa kuanzisha huduma za kusafisha damu (Dialysis) katika hospitali za rufani za mikoa.

Takwimu zinaonyesha kuwa kuna wagonjwa zaidi ya 6,000 wanaohitaji huduma ya usafishaji wa damu, lakini ni wagonjwa 2,100 wanaopata huduma hiyo wengi wao takribani wagonjwa 2,000 wakiwa ni wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Tiba, Dk. Wonanji Vivian, alisema serikali imejipanga kuleta mabadiliko kwenye huduma ya kusafisha damu nchini na Tanzania itakuwa nchi ya kwanza kuwa na gharama za bei nafuu.

"Kwa sababu ya uhitaji mkubwa wa huduma ya dialysis nchini serikali imesogeza huduma hiyo katika hospitali zote za rufani za mikoa na baadhi ya hospitali za halmashauri," alisema.

Alisema huduma ya usafishaji wa damu kwa kipindi kimoja hugharimu kati ya Sh. 240,000 hadi 300,000 na mgonjwa anahitaji vipindi vitatu (vipindi 12) kwa mwezi sawa na gharama ya kati ya Sh. 2,880,000 hadi 3,600,000 kwa mwezi.

"Ili kutatua changamoto hii Bohari ya Dawa ya Taifa (MSD) imechukua hatua ya kuwatafuta watengenezaji wa mashine na kununua moja kwa moja kutoka kwao ili kuondoa gharama za ziada za mawakala," alisema.

Hata hivyo, alisema kufuatia hatua hiyo ya MSD, gharama ya uchujaji wa damu zitashuka na kuwa Sh. 100,000 kwa kipindi kimoja cha sawa na Sh. 1,200,000 kwa mwezi na Sh. milioni 14,400,000 kwa mwaka.

"Mkakati huu utapunguza mzigo mkubwa wa gharama ya huduma ya dialysis kwa wananchi, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na serikali kwa ujumla," alisema.

Mkurugenzi msaidizi wa magonjwa yasiyo ambukiza, Dk. Charles Kihologwe, alisema magonjwa hayo yakiwamo kisukari, shinikizo la damu, figo, yameendelea kuongezeka na vichocheo vikubwa ni mtindo mbaya wa maisha.

"Asilimia 80 ya viashiria huchangia magonjwa hayo kutokana na mtindo wa maisha kama vile ulaji mbaya, ulevi uliopitiliza na kutofanya mazoezi," alisema.

# Magereza yaokoa bilioni 29/- malipo ya wazabuni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza nchini limefanikiwa kuokoa kiasi cha Sh. bilioni 29, ambazo zimekuwa zikilipwa kila mwezi kwa wazabuni wenye tenda za kusambaza vyakula katika magereza mbalimbali nchini.

Pia, jeshi hilo hivi sasa limeanzia utaratibu wa kijitegemea kulisha chakula wafungwa wake zaidi ya 31,000.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa ziara ya kutembelea makao makuu ya jeshi hilo kujionea miradi inayozalishwa, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Suleiman Mzee, alisema fedha hizo zilikuwa zinadaiwa na wazabuni kila mwezi kwa ajili ya kulisha wafungwa wa magerezani.

Alisema hivi sasa wanajitegemea kwa asilimia 90 katika kulisha wafungwa na wameipunguzia serikali mzigo wa madeni kwa wazabuni waliokuwa wakilisha wafungwa nchi nzima.

"Kwa kweli tumeisaidia serikali kuwaondoa wazabuni hivi sasa fedha Sh. milioni 800 za chakula kwa mwezi ambazo zilitolewa na serikali kwa ajili ya chakula zinakwenda kufanya kazi nyingine," alisema Kamishna Jenerali Mzee.

Alisema hivi sasa wanazalisha mazao ya chakula na biashara, pia wanazalisha mbegu za kutosha za alizeti, mahindi na maharagwe ili kuepusha uhaba msimu wa kilimo unapowadia katika magereza mbalimbali nchini.

Kadhalika wamefanikiwa kulipa madeni ya wastaafu 500 ambao walikuwa wanadai na hivi sasa hakuna deni lolote kwa wastaafu.

Alisema wamekuwa na miradi mbalimbali ambayo inawasaidia kuongeza kipato ikiwamo ya matofali ambayo hutumika kujenga nyumba za watumishi pamoja na kuyauza kwa jamii.

Alisema mradi huo ni mzuri na umesaidia kwa kiasi kikubwa kuhakikisha wanatekeleza majukumu ya magereza bila shaka yoyote katika maeneo mbalimbali.

Aliipongeza serikali kwa kuwa pamoja katika shughuli mbalimbali na kuahidi kuwa suala la chakula kwao halina tatizo kwa sababu wanajitegemea wao wenyewe.

Alisema ipo miradi ya mashine, fremu za maduka, kiwanda na mradi wa matofali na kilimo ambavyo vyote ni hazina kubwa katika jeshi hilo kwa sababu vinamanufaa makubwa.

Alisema lengo lao ni kuona jeshi hilo linajitegemea kwa kila kitu kwenye chakula, mavazi na mahitaji mengine wako vizuri na hakuna tatizo lolote.




Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akiwasilisha kwa waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, taarifa ya mafanikio ya sekta ya maji ikiwa ni mwendelezo wa wizara zote kuelezea mafanikio katika kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wafanyakazi TRC, TAZARA waonywa migogoro

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYAKAZI wa Mashirika ya Reli Tanzania (TRC) na Tanzania Zambia (TAZARA) wametakiwa kujiepusha na migogoro katika maeneo yao ya kazi na badala yake wametakiwa kutumia meza ya majadiliano ili kupata suluhu ya kero zao.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini hapa na Mkurugenzi wa Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Lucas Kambelenje, alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Reli Tanzania (TRAWU).

Kambelenje, migomo kazini imekuwa ikishusha uchumi wa Taifa ikiwamo kuleta madhara kwa jamii ambayo inahitaji kupata huduma kutoka mashirika hayo.

Alisema viongozi katika mashirika hayo wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanazima moto wa migomo inapotokea ili kuepusha madhara.

Aliwataka viongozi hao kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Reli (TRAWU) kufanya kazi zao kwa malengo yatakayowasaidia wafanyakazi kwenye maeneo yao ili waweze kujiinua kimapato.

Pia aliwataka viongozi hao kuhakikisha wanatetea maslahi ya wafanyakazi ili waweze kufanya kazi zao kwa uaminifu na kujituma kwa faida ya taifa na wao binafsi. Kwa upande wake mwenyekiti wa chama hicho taifa, Yusuph Mdai, alisema mkutano mkuu upo kwa mujibu wa katiba kwa ajili ya kufanya uchaguzi mkuu wa viongozi wa ngazi ya taifa pamoja na wajumbe wake.

Alisema, katika mkutano huo wanategemea kuwapata viongozi wa ngazi taifa ambao watahakikisha maslahi ya wafanyakazi wa reli nchini yanalindwa.

Awali, akisoma risala kwenye ufunguzi wa mkutano huo, Kaimu Katibu Mkuu TRAWU, Raphael Kazyobi, alisema bado wafanyakazi hao wanakabiliwa na kero mbalimbali zinazokwamisha utendaji wao wa kazi.

Alisema wafanyakazi hao wana mahitaji mengi yanayohitaji kutatuliwa na serikali ikiwamo miundombinu yao ya kazi.

Vile vile, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na serikali katika kuboresha miundombinu yake kwa shirika hilo mazingira yake mengi ya kazi si rafiki kwao.



# Akutwa amejiua kwa kujichoma moto

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MKAZI wa Kijiji cha Ihombe kilichoko Kata ya Utengule Usongwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mashaka Yokonia (35), amekutwa amejiua nyumbani kwake kwa kujichoma moto.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Ulrich Matei, alisema tukio hilo lilitokea Novemba 8, mwaka huu, usiku nyumbani kwake.

Alisema ndugu wa marehemu huyo walibaini kuwa alijiua asubuhi yake ambapo walifika nyumbani kwake na kukuta ameshafariki na kuna mabaki ya vitu alivyotumia kujiunguza.

Kamanda Matei alisema chanzo cha kujiua ni kukata tamaa baada ya kuugua kwa muda mrefu maradhi ambayo hayajulikani na kutelekezwa na mkewe.

Alisema kabla ya kutekeleza tukio hilo alishawahi kujaribu kujilipua kwa kutumia petroli, lakini akaokolewa na mdogo wake, ambaye kwa wakati huo alikuwa jirani.

"Tunaendelea na upelelezi wa shauri hili ili kubaini mambo mengine, tunawaomba wananchi na jamiii kwa ujumla kutoa taarifa endapo watamuona mtu yeyote ambaye anaonyesha kukata tamaa ili wadhibitiwe kabla madhara kama yaliyomkuta Mashaka hayajatokea," alisema Kamanda Matei.

Katika hatua nyingine, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linamshikilia mtu mmoja, Hussein Mohamed (42), mkazi wa Sumbawanga mkoani Rukwa kwa tuhuma za kufanya kazi ya uganga wa kienyeji bila kuwa na kibali. Alisema mtu huyo alikamatwa Novemba 7, mwaka huu, saa 12:15 jioni katika eneo la Iyunga jijini Mbeya akiwa kwenye nyumba ya kulala wageni akiendelea na kazi ya uganga.

Vilevile, alisema jeshi hilo linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kukutwa na dawa za kulevya aina ya bangi kilogramu saba sawa na ujazo wa debe mbili na kete 315.

Aliwataja watu hao ni Expedito Makunga (38), mkazi wa Mlowo mkoani Songwe na Ngala Mayombo (30), mkazi wa Ifakara mkoani Morogoro.

Alisema watu hao walikamatwa Novemba 8, mwaka huu, saa 01:30 usiku katika Kitongoji Matanda, Kijiji cha Itumbi wilayani Chunya na kwamba watuhumiwa ni wauzaji na watumiaji wa dawa hizo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kulia), akijadiliana jambo na wakuu wa Wilaya wa Rungwe, Dk. Vicent Anney (katikati) na Kyela, Ismail Mlawa, baada ya kikao cha kujadili mikakati ya kuboresha zao la cocoa, jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Halmashauri zazawadiwa ng'ombe ujenzi madarasa

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewaahidi watumishi wa halmashauri na wilaya zilizofanya vizuri kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa kupewa motisha ikiwamo zawadi ya ng'ombe.

Homera alitoa kauli hiyo jana wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya wakati akizungumza na madiwani pamoja na watumishi.

Homera alisema Serikali ya Mkoa wa Mbeya ilipokea Sh. bilioni 15 ya fedha za Uviko-19 kutoka serikalini ili zitumike kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo sekta ya elimu, afya na maji.

Alisema hadi kufika Novemba 30, mwaka huu, kwa mujibu wa maelekezo kila halmashauri na wilaya inatakiwa kukamilisha vyumba vya madarasa.

Halmashauri itakayowahi kukamilisha vyumba vya madarasa lazima tuwazawadie ng'ombe achinjwe watu wanywe supu na kufurahia kazi nzuri waliyoifanya, muhimu zaidi msingatie matumizi bora ya fedha zilizotolewa ili ziendane na miundombinu inayojengwa," alisema Homera.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa, alimhakikishia Homera kwamba ujenzi wa vyumba vya madarasa unaendelea vizuri na kwamba kabla ya Novemba 30 utakamilika.

Aidha, katika kikao hicho baadhi ya madiwani waliiomba serikali kuboresha miundombinu ya mawasiliano ya simu ambayo kwa sasa ni tatizo kubwa wilayani Kyela.

Diwani wa Njisi, Omary Rashid, alisema hakuna mawasiliano ya simu katika kata yake na maeneo mengine ya wilaya hiyo hali inayokwamisha utekelezaji wa shughuli zao za kila siku.

Aliiomba serikali kushughulikia kwa haraka ili wananchi wapate huduma za mawasiliano kama ilivyo maeneo mengine kuliko sasa ambapo mitandao ya nchi jirani ya Malawi ndio yenye nguvu maeneo hayo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, aliwaahidi madiwani kushughulikia kwa haraka kwa kufanya mazungumzo na wamiliki wa mitandao ya simu ili kuboresha huduma za mawasiliano wilayani Kyela.

# Wabomoa wenyewe kupisha ujenzi shule

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mtaa wa Iduda Kata ya Iziwa jijini Mbeya wamelazimika kubomoa makazi yao na kufyeka miti ikiwapo ya matunda bila kulipwa fidia kufuatia agizo la Mkuu wa Wilaya, Dk. Rashid Chuachua.

Walifanya hivyo baada ya kuelezwa kilochoelezwa kupisha mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kata.

Wakizungumza na Nipashe juzi wananchi hao walisema zaidi ya kaya tano zenye makazi, mazao ya miti na matunda, zimeumizwa na kitendo hicho kwani makazi yao yalijengwa tangu mwaka 1983 na hawajui wataishi wapi na familia zinazowategemea.

Stephano Mwasyoge alisema kuwa kitendo cha serikali kutotoa fidia kimewaweka njia panda na kumwomba Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kuingilia kati na kuona namna ya kuwasaidia.

"Kwa mfano, kama mimi eneo nililojenga lilikuwa la wazazi wangu, nimeishi miaka 45 sasa sielewi naanzia wapi na nitaenda wapi na watoto ambao wanashindwa hata kuhudhuria masomo," alisema.

Alisema kuwa hawapingani na serikali kupisha eneo hilo kwa ajili ya mradi wa shule ya sekondari ya kata bali wanaomba kuonewa huruma kutengewa maeneo na kulipwa fidia.

Mjane Laeli Kihobeli, aliiomba serikali kuingilia kati na kwamba eneo lake alipanda mazao ya miti ambayo imekuwa ikikatwa bila utaratibu.

China Mazonje alisema kuwa licha ya kumwomba Mkuu wa Wilaya kulipwa fidia bado aliwapa siku saba wawe wamebomoa makazi yao na kuwaeleza hakuna fidia.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alisema ni kweli wameagizwa kubomoa kupisha mradi wa shule ya sekondari ya kata.

Alisema eneo hilo tangu mwaka 1983 limetengwa kwa ajili ya shughuli za kijamii na suala la fidia hawapaswi kulipwa kabisa.

"Tunavyo vielelezo vyote vya eneo hilo na hakuna aliyeonewa sasa wanapaswa kupisha mradi ambao utakuwa chachu kwa watoto wao kupata elimu bora na eneo hilo idadi kubwa yalikuwa ya wazazi wao," alisema.

Kwa upande wake mwanaharakati wa haki za binadamu, Raphael Ngonde, alisema kuwa kitendo cha mkuu wa wilaya kutoa siku saba bila fidia ni kinyume cha taratibu za sheria za ardhi.

## Walalamikia mifumo mibovu maji machafu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wanaokaa katika nyumba mpya zilizojengwa na serikali katika Kijiji cha Dunduwa, Wilaya ya Kaskazini B', Unguja, wamelalamikia mifumo ya karo za choo na maji machafu kutofanya kazi vizuri.

Wakizungumza jana na Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B, Unguja, wakazi hao walisema kero hiyo ya karo inawasababishia usumbufu mkubwa kutokana na kinyesi kutokwenda sehemu husika.

Fatma Ali Khamis na Abdalla Mussa, miongoni mwa wananchi hao, walisema baadhi ya nyumba wameshindwa kutumia huduma za vyoo kwa baadhi ya matumizi na kusababisha kufuata huduma hizo katika nyumba ya ibada ambayo iko karibu na kijiji hicho.

Fatma alisema uwapo wa shimo moja la karo linalotumiwa na nyumba zipatazo nane, husababisha usumbufu mkubwa kwa sababu mifumo ya usambazaji wa kinyesi haipo sawa.

"Ni shimo moja tu pekee ndilo linalopokea kinyesi na linashindwa kupeleka uchafu katika shimo lingine jambo ambalo limesababisha shimo hilo kujaa," alisema Fatma.

Pia alisema licha ya kuwa na hofu ya kupata maradhi ya mlipuko lakini tayari baadhi ya wanakijiji wamekumbwa na maradhi ya matumbo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya hiyo, Hamid Seif Said, alisema atawasiliana na wahusika wa nyumba hizo ili kuhakikisha kuwa matatizo yao yanatatuliwa.

Wakati huo huo, Hamid alifanya ziara katika mashimo mbalimbali ya mchanga yaliyoko Bumbwini na kulaani vitendo vya uchimbaji wa mchanga holela.

Ofisa Mazingira wa Wilaya hiyo, Mashavu Khamis Khatib, alisema wanaochimba mchanga wanakiuka baadhi ya taratibu za mita za kuchimba na kwenda kina kirefu kinyume cha utaratibu wa uchimbaji.

# Mcheza filamu India apania kutangaza utalii wa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWIGIZAJI nyota wa filamu za Kihindi, Sanjay Dutt, amesema azma yake ni kuwekeza katika sekta mbalimbali za maendeleo zikiwamo utalii, afya, miundombinu, sanaa na filamu.

Pia amesema anatarajia kutoa huduma kwa jamii hasa kwa wale wanaoishi katika mazingira magumu.

Sanjay aliyasema hayo juzi Ikulu Zanzibar wakati akizungumza na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Msanii huyo wa filamu nchini India, alisema kisiwa cha Pemba ni eneo ambalo atalitumia kwa ajili ya uwekezaji hasa katika sekta ya utalii.

Alisema kisiwa cha Pemba kinafanana na kisiwa cha Bahamas nchini India na kina fursa nyingi za uwekezaji hasa sekta ya utalii ambayo itasaidia kukifungua kisiwa hicho.

Pia aliahidi kwamba pia atasaidia jamii katika sekta za elimu, nyumba nafuu na afya na kutengeneza fursa mpya za ajira.

"Zanzibar na India zina uhusiano wa zaidi ya karne moja hali ambayo imetoa fursa kwa wananchi wa pande hizo mbili kuishi pamoja na kutembeleana kwa shughuli mbalimbali ikiwamo matibabu," alisema.

Nyota huyo alieleza azma yake ya kuanzisha kampuni ya filamu Zanzibar na kuifanya Zanzibar kuwa sehemu mojawapo ya kuigiza filamu zake kupitia kampuni yake.

Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi, alisema serikali anayoiongoza itampa kila ushirikiano katika kuhakikisha azma yake hiyo inafanikiwa na mipango yote aliyoipanga kwa Zanzibar inakwenda sawa.

Alisema serikali imedhamiria kukifanya kisiwa cha Pemba kuwa sehemu maalum ya uwekezaji na jinsi ilivyoweka mikakati ya kuhakikisha hilo linatekelezwa baada ya nyota huyo kueleza jinsi alivyovutiwa na mazingira ya kisiwa hicho.

Rais Dk. Mwinyi alimweleza mwigizaji huyo kuwa ujio wake una umuhimu mkubwa katika kuutangaza utalii wa Zanzibar pamoja na vivutio vilivyopo huku akitumia fursa hiyo kumweleza dira ya uchumi wa Zanzibar hivi sasa ambayo ni uchumi wa bluu na inavyokwenda sambamba na sekta ya utalii.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohammed Mussa, alisema ikiwa mwigizaji huyo atarekodi filamu zake nchini, Zanzibar itanufaika na itaendelea kujulikana zaidi duniani hasa bara la Asia.

Alisema bara la Asia ni soko ambalo bado halijazoeleka sana, hivyo kupitia mwigizaji huyo ambaye anajulikana duniani kote atasaidia kwa kiasi kikubwa kuifungua Zanzibar katika soko hilo.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar anayeshughulikia Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali (kushoto), akipatiwa maelezo kuhusu hifadhi ya jamii, alipotembelea banda la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, (PSSSF) kwenye Maonyesho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ yaja na mkakati kurejesha watoto shuleni

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKURUGENZI wa Elimu Mbadala na Watu Wazima kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mashavu Ahmada Fakih, amesema kutokana na kuwapo wimbi kubwa la watoto waliotoroka shule, serikali imeona ni lazima kuhakikisha watoto hao wanarudi shuleni kuendelea na masomo.

Amesema imeonekana wengi wao wamekuwa wakidhalilishwa na kujihusisha na ajira za utotoni hali ambayo inawanyima haki yao ya msingi kikatiba na kupoteza nguvu kazi ya taifa.

Akizungumza jana katika mkutano maalumu na madiwani wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, katika ukumbi wa Baraza la Mji Kaskazini B, ulioko Kinduni, alisema mradi wa kuwarejesha watoto shuleni unaunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha watoto wote wanapata haki yao ya elimu, hivyo ni vyema wadau wote kushirikiana katika kufanikisha azma hiyo.

Utaratibu wa kuwarejesha watoto shuleni, alisema haukuanza kipindi hiki bali tangu mwaka 2000 na serikali imeweka idara maalum ya elimu mbadala na watu wazima kwa lengo la kuwasaidia vijana waliokosa elimu, kuendelea na masomo yao.

Alisema katika mkoa wa Kaskazini Unguja, kuna watoto 6,477 ambao wako nje ya masomo, hivyo ni lazima madiwani kushirikiana na masheha, wakuu wa wilaya na wazazi kuhakikisha wanawarejesha watoto hao shuleni.

Akifungua mkutano huo, Mkurugenzi wa Baraza la Mji Kaskazini B, Abdulrahman Ali Mukhtari, alisema ushirikiano wa pamoja unahitajika katika kuhakikisha mradi huo unafanikiwa.

Aliwashauri wazazi na walezi kuwafuatilia watoto katika masomo yao na kuwa karibu na watoto wao ili kuwalinda na masuala mbalimbali yakiwamo ya udhalilishaji. Akiwasilisha ripoti ya utafiti ya mradi huo, Mzee Shirazi alisema watoto 35,732 kwa Zanzibar nzima wako nje ya mfumo wa masomo idadi ambayo ni kubwa hasa ikizingatiwa kuwa watoto hao ndio tegemeo kubwa la taifa.

Mzee alisema mradi huo unalenga watoto walio na umri wa miaka saba hadi 14, lakini haimaanishi kama wapo watoto waliokuwa zaidi ya umri huo wasipelekwe shule, bali ni vyema kuwapeleka ili kuendelezwa na elimu kutokana na umri wao.

Alisema ushirikiano mzuri umeanza kupatikana na tayari watoto 3,200 wamesharudi shuleni ambao tayari wameshasajiliwa rasmi, huku wakiwa na madarasa 82 ya watoto hao.

Pia alisema mradi huo unalenga kuwapa mafunzo walimu maalumu ambao ni wa kujitolea kuwasaidia watoto hao kwa kuwaweka vizuri ili wasitoroke tena, pamoja na kuwapa posho lao ili kuwasaidia kujiendeleza wao wenyewe kimaisha.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAPPINESS GUIDO MSITA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P2533/0007** kilichotolewa na abaraza la mitihani kupitia kituo/shule ya secondary ya **SAMBU** mwaka **2015,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DSM/PHQ/RB/535452/2021**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**JUMA YUSUPH MAKOTA** anatangaza kupotelewa na result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S0600/0526** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **BUNDA mwaka 2021,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/KIG/RB/527919/2021**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**REHEMA HASSAN MBULALINA** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **AB738448** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka **2015.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHU/RB/536115/2021.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**CHRISTINA EDWIN MALEMA** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba S.0211/0846 iliyotolewa na LOLEZA SEKONDARI mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MBU/RB/514434/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

ATHUMAN BAKARI ATHUMAN Anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya PIKIPIKI aina ya BOXER yenye namba za usajili MC 125 CMU. Kwa yeyote atakaeiona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Rb Namba. MOR/MOR/ RB/389550/2021.

---

**UTAMBULISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI KATIKA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**IRINGA**

**SHAURI NA: 2/2021**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRADHI YA MAREHEMU.............LUCAS HALE MWAKABUNGU**
**NA**
**MUOMBAJI......CAROLINE LUCAS MWAKABUNGU**

**FOMU 58**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Miradhi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi wa Miradhi kwa Muombaji aliyetajwa hapo juu.
Pingamizi kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 30/11/2021.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 9/11/2021.

S. R. Ding'ohi
Naibu Msajili
Mahakama Kuu ya Tanzania
IRINGA

116564402

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**ARUSHA**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 29 LA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**JOSIAH ALPHAYO**
**LETARA……………MAREHEMU**
**NA**
**LOIRUK JOSIAH LETARA……..MWOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**KANUNI YA 75**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimammizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 17 mwezi wa pili mwaka wa 2022
**Imewasilishwa arusha leo tarehe 04/11/2021**

R. B. Massam
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
ARUSHA.

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP JUDICIAL CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 142 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late KARLO ALBERT SENDWA**

**and**

**In the Matter of Application for letters of administration by DEVOTHA PROSPER KINABO AND NAOMI KARLO SENDWA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner. Objections to the grant should be filed on or before the 24th of November, 2021.
**Dated at Dar es salaam this 10th day of November,** 2021.

Registrar/Senior Resident Magistrate

116564602

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa Njombe**

**Usimamiziwa mrathi Na 102, 2021**

**Katika shauri la mirathi ya OWEN JAPHET KILASI......................Marehemu Wa NJOMBE**

**Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa na ADELA SEVERIN MLIGO ......Mwombaji.**

**TANGAZO KWA UMMA.**

**(Kanuniya 5(2) yakanuni za usimamizi wa Mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuudhuria katika shauri hili endapo wakita kakufanya hivyo mnamo tarehe ...23.......mwezi ...11..... mwaka... 2021..... kabla ya huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo ,mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpakata rehetajwa hapo juu.
Zingatia;Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
*Marehemu hakuacha wosia
*Futa isiyohusika
Imetolewa leo tarehe...10.... mwezi ...11.... Mwaka...2021.....

HAKIMU MKAZI

116564702

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**ARUSHA**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 29 LA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**HELENA JOSIAH**
**LETARA……………........MAREHEMU**
**NA**
**LOIRUK JOSIAH LETARA….……..MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**KANUNI YA 75**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimammizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 10 mwezi wa pili mwaka wa 2022
**Imewasilishwa arusha leo tarehe 05/11/2021**

R. B. Massam
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
ARUSHA

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**EMMANUEL MUSOMA JIHILA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 124 CCN** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **GEI /MBO/ RB/679543/2020**

116565302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**KISHEGENA TRANSPORT COMPANY LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI AINA YA TRAILER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 696 BCH** NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA IST** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T467 CEJ** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/ RB/553/2021**

116565402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YOSIA RAMECK POTEZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA SUCCEED** yenye namba za usajili **T 197 DQU.** Chassis **No. NCP510148535,** Engine No. **1N2C382404.** Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/533425/2021.**

116565502

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**EMMANUEL OBEDI MNYALIVA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina **MOHAMMED ENTERPRISES (T) LTD** aina ya **BAJAJ BOXER** yenye namba za usajili **MC 515 CJX.** Chassis No. **MD2A21BYXRWF99798,** Engine **No. PFZWKF31095.** Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOD/MPW/RB/537350/2021.**

116565602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHABBY MAKAPANE MAKAPANE** Anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya Gari yenye namba za usajili **T269DGX.** Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Rb Namba. **MOR/MOR/RB/534690/2021.**

116565702

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Waliotimuliwa CUF kwenda kwa msajili

Na Enock Charles

WALIOKUWA viongozi katika Chama cha Wananchi (CUF) na kuvuliwa uongozi pamoja na uanachama, wametangaza kwenda kwa msajili wa vyama vya siasa kudai kile walichokiita tafsiri ya uamuzi uliofanyika.

Wamedai hatua hiyo inatokana na ukiukwaji wa taratibu katika chama hicho zilizosababisha kuvuliwa uongozi na uanachama.

Wakizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, viongozi hao akiwamo aliyekuwa Mkurugenzi wa Habari na Uenezi, Abdul Kambaya, walidai utaratibu uliotumika kuwavua uanachama haukufuata misingi ya Katiba ya chama hicho ikiwamo kutotimia kwa akidi ya wajumbe na kuingizwa kwa wajumbe wasiokuwa halali.

"Tutapelekea malalamiko yetu kwa msajili kuomba tafsiri ya zile ibara zilizokiukwa ndani ya kikao cha Baraza Kuu, tunafanya haya kukinusuru chama na kulinda heshima ya chama chetu," alisema Kambaya.

Kambaya aliukosoa uongozi wa chama hicho kwa kile alichodai kutokubali kukosolewa na kufuata misingi ya Katiba wakati kimekuwa kikitaka Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CC) kufuata Katiba na kukubali kukosolewa, jambo ambalo linawafanya kuonekana hawana msimamo.

Aliyekuwa Mbunge wa Mchinga 2015-2020, Hamidu Bobali, ambaye hakufukuzwa bali alipewa karipio kali, alilalamikia kutokupewa nafasi ya kusikilizwa kabla ya kupewa adhabu hiyo akisema kitendo hicho kinaonyesha kutokufuatwa kwa misingi ya demokrasia duniani inayotaka mtu kupewa haki ya kusikilizwa kabla ya kuhukumiwa.

Pia alidai Kamati ya Maadili ilikaa bila ya kuwapo kwa mwanasheria kama inavyotakiwa kikatiba.

"Mimi sikuitwa kwenye baraza kuu kwenda kuhojiwa, wenzangu waliitwa, kikao kimekaa kimepokea taarifa ya upande mmoja hakikutaka kunisikiliza hoja zangu mwishoni wakanihukumu," alisema Bobali.

Akijibu madai hayo, Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho bara, Magdalena Sakaya, alisema kuwa siyo kweli kwamba taratibu zilikiukwa na kusisitiza kuwa zilifuatwa ikiwamo kuwa na wajumbe halali waliotakiwa na kutimiza akidi kama Katiba ya chama hicho inavyoelekeza.

"Kikao cha maadili siyo lazima kiwe na mwanasheria kina wajumbe watano wa lazima ambao ni Makamu Mwenyekiti Bara, Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Naibu Katibu Mkuu Bara, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar na Mkurugenzi wa Itifaki na Mafunzo, wajumbe watatu wanaoweza kuongezwa mwenyekiti akipenda," alisema Sakaya.

Kuhusu madai ya Bobal, Sakaya alisema siyo kweli kwa kuwa kada huyo aliitwa katika Kamati ya Maadili na kusikilizwa na baada ya hapo alikiri makosa yake na kuomba msamaha.



Meneja wa Mfuko wa Dhamana kwa Wateja Wadogo wa Benki ya Kilimo Tanzania (TADB), Asha Tarimo (kushoto), akitoa maelezo kuhusu faida ya kutumia benki hiyo kwa mteja Yahaya Duru aliyetembelea banda la benki hiyo, katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Kifedha kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Polisi waendelea na uchunguzi waliotekwa

Na Mwandishi wetu

JESHI la Polisi mkoani Lindi, limesema kuwa linaendelea na upelelezi wa tukio la wanaume watano wanaodaiwa kutekwa na watu wasiojulikana na muda utakapowadia watatoa taarifa kamili.

Akizungumza jana na Nipashe kwa njia ya simu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Foka Dinya, alisema; "Bado tunaendelea na uchunguzi wetu wakati ukifika tutasema."

Alipoulizwa kama jeshi hilo limeshajua waliowateka watu hao alisema "Hatujajua nani kawateka ila tunaendelea na uchunguzi."

Wanaume hao walitekwa na watu wasiojulikana wanaokadiriwa kuwa saba ambao walifika kwenye makazi yao usiku wakiwa na silaha na kuwaamuru kuamka kisha kuwapekuwa na kuchukua kadi zao za benki na kuondoka nao kusikojulikana.

Wanaodaiwa kutekwa na kupelekwa kusikojulikana ni Isumail Uwesu Yahaya, Shazir Mohamedi Chileu, M'baraka Ally Maliki, Hamisi Said Liendeko, wote wakazi wa Kijiji cha Rutamba ya sasa na Mussa Fukutu wa Kijiji cha Michee.

Wengine ni Husuna Mohamedi, Esha Mohamedi na Husuna Issa.

Jumatatu ndugu wa waliotekwa walisema kuwa watu hao wakiwa na silaha walifika kwenye kila nyumba na kugonga mlango na kuwachukua wanaume, huku wanawake wakitakiwa kuendelea kulala na hadi sasa hawajui ndugu zao walipo.

Mwenyekiti wa Serikali ya vijiji vya Rutamba ya sasa na Michee, Abdurahamani Awadhi walikiri kwa wananchi wao kutekwa nyara na kueleza hadi kufikia sasa bado hawajaweza kufahamu eneo walikopelekwa ndugu zao, licha ya kupita kuulizia vituo mbalimbali vya polisi bila mafanikio.

# Majaliwa: Serikali kuendeleza uwiano kijinsia katika uongozi

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha inajenga uwiano mzuri wa kijinsia na wanawake katika uongozi na ngazi nyingine za maamuzi.

"Nitumie fursa hii pia kutambua mchango mkubwa wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kujenga uwiano wa kijinsia na wanawake katika uongozi".

Alisema hayo jana alipomuwakilisha Rais Samia katika ufungaji wa Jukwaa la Uongozi wa Vijana kwa mwaka 2021, lililofanyika katika Chuo cha Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa (MS TCDC), jijini Arusha.

Alisema katika uteuzi alizozifanya hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, aliteua majaji wanawake 13 kati ya 28 wa Mahakama Kuu sawa na asilimia 43 na kufanya idadi ya majaji wote nchini kufikia wanawake 40 kati ya wote 86. "Ukiachilia mbali Katibu wa Bunge mwanamke, Mheshimiwa Rais pia aliteua Makatibu Tawala wa Mikoa wanawake 12 kati ya 26 sawa na asilimia 46".

Majaliwa alisema Tanzania imeendelea kupiga hatua kubwa kuhakikisha inajenga uwiano mzuri wa kijinsia na wanawake katika uongozi na ngazi za maamuzi.

"Kwa mfano katika uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani wa mwaka 2015, tulikuwa na wabunge wanawake 127 ikilinganishwa na wabunge wanawake 143 mwaka 2020."

Alisema ili kukabiliana na changamoto ya ajira Tanzania iliamua kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kujenga uchumi wa kati wa viwanda na kutengeneza ajira kwa kufungamanisha sekta hiyo na sekta nyingine za uchumi ikiwamo kilimo, madini, maliasili na utalii na sekta ya ujenzi.

Vile vile, alisema juhudi hizo zimeonesha mafanikio baada ya Julai, 2020 Tanzania kuingia kwenye kundi la nchi zenye uchumi wa kati wa chini.

Alitoa wito kwa kwa wakuu wa nchi na Serikali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Umoja wa Afrika na sekta binafsi kuongeza juhudi katika kujenga usawa wa kijinsia na wanawake katika uongozi na ngazi nyingine za maamuzi.

Pia, alisema serikali inatambua mchango wa vijana wa kukuza uchumi na kwamba ni muhimu vijana wakaendelea kujituma, kujitoa, na kuwa waadilifu ili kujenga taifa adilifu hasa wanaposhiriki katika matukio mbalimbali ya uzalishaji mali.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Peter Mathuki, alisema atahakikisha anayafikisha mawazo yote yaliyotolewa na vijana hao kwa watunga sera katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili yaweze kufanyiwa kazi kwa maendeleo ya vijana na jumuiya kwa ujumla.

Kadhalika, aliwaomba viongozi mbalimbali waendelee kuwafundisha na kushirikiana na vijana hao ili waweze kujifunza zaidi na kuwa viongozi bora hapo baadaye.

HABARI MICHEZO

# BARAZA AKIRI LIGI KUU BARA BORA ZAIDI AFRIKA MASHARIKI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar iliyopo nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, Mkenya Francis Baraza, amelikubali soka la Tanzania baada ya kukiri kwamba linazidi kuwa imara na ubora wa wachezaji wake umeongezeka maradufu na hakuna tofauti kama ilivyokuwa awali kwa ubora wa wachezaji wa nchini Kenya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema awali kulikuwa na dhana iliyojengeka kuwa wachezaji na ligi ya Kenya ni bora huku wachezaji wengi kutoka nchini humo wakipata nafasi ya kusajiliwa na kucheza soka Tanzania.

Alisema kuwa misimu hii karibuni imekuwa tofauti kwa sababu haoni tofauti kubwa kati ya wachezaji wa hata Ligi ya Tanzania na Kenya.

**"Kwangu sioni kama kuna tofauti kubwa, kitambo kulikuwa na msemo eti wachezaji wa Kenya wanatumia mpira wa nguvu kuliko wa Tanzania, lakini kwangu naona ni sawa na Tanzania wamekuwa bora kidogo kulingana na ligi yao," alisema Baraza.**

Alisema kuhusu uendeshaji wa Ligi ya Tanzania na Kenya, ni vitu viwili tofauti, lakini kwanza akawapongeza wasimamizi wa Bodi ya Ligi nchini (TPLB) kwa kufanya kazi kubwa ya upangaji wa ratiba.

"Kwa kweli uendeshaji wa ligi humu ni Kenya ni vitu viwili tofauti, kwanza nitawapongeza sana wasimamizi wa bodi ya ligi humu nchini, Tanzania timu ziko umbali mkubwa, lakini wasimamizi wa ligi wamejaribu mno kuwezesha mechi zote kupangwa kwa wakati unaofaa ili kusiwe na timu zIngine kuwa na malalamiko," alisema Baraza.

Alisema kuhusu ushindani wa ligi kwa nchi hizo mbili, huwezi kulinganisha kwa sasa kwani Tanzania imepiga hatua kubwa sana kwa sababu ya wadhamini kumwaga mamilioni ya shilingi.

"Tanzania imepiga hatua kubwa mno kimpira kutokana na wadhamini kumwaga zawadi kwa wingi kwa mshindi, hicho tuu kimefanya ligi ya Tanzania kuwa bora Afrika Mashariki na Kati," alisema Baraza.

## BADO MLANDEGE...



Wachezaji wa Yanga wakiendelea na mazoezi ya viungo gym jana asubuhi, wakijiandaa na mechi ya pili ya kirafiki dhidi ya KMKM FC itakayopigwa kesho katika Uwanja wa Amaan Zanzibar baada ya juzi usiku kuichapa Mlandege FC bao 1-0 uwanjani hapo. **PICHA: YANGA**

## Yanga yampeleka Yacouba kutibiwa

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Yanga raia wa Burkina Faso, Yacouba Songne, amepelekwa nchini Tunisia kwa matibabu ya majeraha aliyoyapata kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting.

Taarifa iliyotolewa na klabu ya Yanga jana kupitia mtandao wake rasmi wa kijamii Instagram ilieleza kuwa mchezaji huyo ambaye wakati mwingine hucheza kama winga, ameambatana na daktari wa viungo, Youseef Mohamed kuelekea Tunisia kwa matibabu hayo.

"Klabu ya Yanga imempeleka mchezaji Yacouba Songne nchini Tunisia kufanyiwa matibabu ya majeraha aliyoyapata kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Ruvu Shooting. Yacouba, ameambatana na daktari wa viungo Youseef Mohamed," Ilieleza taarifa hiyo.

## Kocha Kisiwani atoa sababu vipigo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KUPOTEZA michezo mitatu ya Ligi Kuu Zanzibar (Ligi Kuu ya PBZ), sababu haiwezi kuwa ni kutokana na wachezaji kuwa wageni kwenye ligi hiyo, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa timu ya Kisiwani FC, Khatib Omar Salum.

Kisiwani inashuka dimbani leo, dhidi ya Maafande wa Mafunzo, mchezo utakaopigwa katika Dimba la Mau A majira ya saa 10 alasiri ikiwa ni mchezo wa mzunguko wa nne wa Ligi Kuu ya PBZ.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Salum alisema kwa sasa hawezi kuwatetea wachezaji wake kuwa kufungwa mechi tatu mfululizo kumetokana na ugeni wao katika ligi hiyo yenye ushindani mkubwa, bali tatizo ni kushindwa tu kuhimili mikiki ya Ligi Kuu.

# *Sanjay Dutt aahidi kukuza filamu nchini*

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa, amekutana na kufanya mazungumzo na mwigizaji mashuhuri wa filamu za Kihindi kutoka nchini India, Sanjay Dutt, ambaye ameahidi kushirikiana na serikali katika kukuza tasnia ya filamu nchini.

Katika mazungumzo hayo yaliyofanyika jana ofisi ndogo ya Waziri Mkuu, Magogoni jijini Dar es Salaam, Majaliwa aliahidi serikali kumpa ushirikiano wote kuhakikisha msanii huyo anatimiza malengo ya ziara yake nchini.

Waziri Mkuu pia alitumia fursa hiyo kuwataka wadau wa filamu nchini kutumia ujio wa msanii huyo mkubwa duniani kuimarisha uhusiano pamoja na kujifunza namna bora ya kuboresha kazi zao kupitia yeye na kuweka mipango ya kufanya kazi kwa pamoja.

Pia, Waziri Mkuu alimshukuru msanii huyo ambaye pamoja na mambo mengine ameahidi kushirikiana na Bodi ya Filamu Tanzania katika kuendesha mafunzo ya masuala mbalimbali katika tasnia hiyo ikiwamo uandaaji wa filamu kwa kutumia teknolojia ya kisasa hususan kwa vijana.

Kwa upande, Dutt alisema amevutiwa na fursa nyingi zilizoko kwenye sekta ya utalii nchini na kuahidi kuvitangaza vivutio hivyo na kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa kwenye ramani ya dunia katika masuala ya utalii.

Mbali na ahadi hiyo, pia msanii huyo amesema atashirikiana na wadau wa filamu nchini wakiwamo waandaaji pamoja na waigizaji kutoa mafunzo na mbinu bora zitakazowawezesha kuboresha kazi zao na hatimaye kupata mafanikio zaidi.

Amesema katika ziara yake anatarajia kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii ambapo atapiga picha kwa ajili ya kuvitangaza ili kuwavutia watu wengi waje Tanzania. Miongoni mwa vivutio hivyo ni pamoja na mbuga za wanyama za Serengeti na Ngorongoro.

"Jana nilikuwa Zanzibar, nimeona fursa nyingi za uwekezaji hapa Tanzania ikiwamo uwapo wa fukwe nzuri. Nitakwenda kuwashawishi marafiki zangu nao waje kuwekeza. Naipenda sana Tanzania watu wake ni wakarimu na ninatarajia kuja kufanya filamu," alisema.

Wakati huo huo, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Innocent Bashungwa, amesema kupitia ujio wa Dutt, wizara yake inategemea kuangalia maeneo ya kimkakati ambayo wanaweza kushirikiana na msanii huyo ikiwamo uandaaji wa filamu, kuongeza wigo wa masoko ya filamu na matumizi ya teknolojia katika kuikuza sekta ya filamu nchini.

Aliongeza kuwa kupitia Chuo cha Sanaa Tanzania (TaSUBa), Dutt ametoa ushauri wa namna bora ya kushirikina ikiwamo kutoa mafunzo kwa wasanii na waandaaji wa filamu.

## ZISIKUPITE

### POGBA KUUZWA JANUARI

MANCHESTER United wanajiandaa kumuuza kiungo wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba, 28, katika dirisha la Januari. ***(Star)***

### RAMSEY AWANIWA EVERTON

KLABU ya Everton na Newcastle United zinataka kumsajili kiungo wa kati wa Juventus na Wales, Aaron Ramsey, 30. ***(Goal)***

### COUTINHO ASHUTUMIWA BARCA

NYOTA wa Barcelona wamechukizwa na kiungo wa kati wa Brazil, Philippe Coutinho, 29, wakimshutumu mchezaji huyo kwa kuzembea huku kukiwa na tetesi za kuhamia Newcastle United. ***(Star)***

### BOWEN ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL wanamtaka winga wa West Ham, Jarrod Bowen, 24, na wanapanga kumsajili Januari. ***(Mirror)***

### SEVILLA NA DAU LA KOUNDE

KLABU ya Sevilla imesisitiza kwamba, Jules Kounde, 22, hataruhusiwa kuondoka kwa chini ya euro milioni 80. ***(AS)***

### SHEVCHENKO AMTAKA PULISIC

KOCHA mpya wa Klabu ya Genoa Andriy Shevchenko anataka kumsajili mshambuliaji wa Chelsea na Marekani, Christian Pulisic, 23. ***(Secolo XIX)***

### DEMBELE NA NEWCASTLE

Newcastle United huenda wakampata Mfaransa Ousmane Dembele, 24, kwa uhamisho wa bila malipo ikiwa winga huyo atakataa kusaini mkataba mpya na Barcelona. ***(Express)***

### LODGERS ATAJWA UNITED

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers anapigiwa upato kuchukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer kama kocha mpya wa Manchester United. ***(Eurosport)***

### MESSI KURUDI BARCA

BARCELONA huenda wakamsajili tena mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, 34, mwaka 2023 wakati mkataba wake na Paris St-Germain utakapomalizika, amesema mgombea wa urais wa zamani wa klabu hiyo, Victor Font. ***(Marca)***

### SULE ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United wameanza kufanya mazungumzo na wawakilishi wa beki wa Bayern Munich na Ujerumani, Niklas Sule, 26. ***(Newcastle World)***

### KOUNDE ANUKIA MAN UTD

MANCHESTER United wana matumaini ya kuishinda Chelsea katika harakati za kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Jules Kounde, 22, kutoka Sevilla. ***(AS via Express)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI AUNDA JOPO LAKE, ATIMUA MAKOCHA WA2

**Kisa ni wachezaji kuchoshwa na ongezeko la majeruhi na kuwanyooshea vidole wakufunzi wa...**

**BARCELONA,** Hispania

SIKU moja baada ya kutambulishwa rasmi kuwa Kocha Mkuu wa Klabu ya Barcelona mbele ya mashabiki 10,000, Xavi Hernandez amewatimua makocha wawili.

Klabu hiyo ya Katalunya imekumbwa na wimbi la majeruhi na kusababisha mgawanyiko kati ya wachezaji na viongozi huku timu ikiachwa mbali dhidi ya wapinzani wao Real Madrid kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

**Gazeti la kila siku la AS la Hispania, limesema tangu alipoteuliwa Xavi Novemba 7, mwaka huu ameshuhudia mabishano na ameamua kuchukua hatua, akiwaambia kocha wa viungo, Juanjo Brau na daktari Albert Roca waliowasili pamoja na kocha aliyetimuliwa Ronald Koeman kwamba hawahitajiki tena Barca.**

Imeripotiwa kuwa wachezaji wamechoshwa na ongezeko la majeruhi na wanawanyooshea vidole wakufunzi hao wa mazoezi ya mwili wakiamini matatizo yao yalianza wakati wa mechi za kujiandaa na msimu wa ligi na yameendelea.

Ripoti hizo zimedai Xavi atawarejesha katika klabu hiyo Jaume Munill na Ricard Pruna kusaidia kutatua tatizo linaloendelea la majeruhi ikitiliwa maanani jinsi wakufunzi hao wawili walivyofanya kazi awali hapo Nou Camp.

MECHI KALI

HOME AWAY

TANZANIA
2.85 | 2.99 | 2.41
DR CONGO

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 667

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# GERRARD, TERRY, LAMPARD WATAJWA ASTON VILLA

**LONDON,** England


KLABU ya Aston Villa walimfungashia virago Kocha wao, Dean Smith na kufanya awe ni kocha wa tano msimu huu kutimuliwa na klabu za Ligi Kuu England, baada ya Xisco Munoz (Watford), Nuno Espirito Santo (Tottenham) , Steve Bruce (Newcastle) na Daniel Fark (Norwich) kufutwa kazi.

Sasa wachezaji wa zamani wa timu ya Taifa ya England, John Terry, Steve Gerrard na Frank Lampard wote wamehusishwa na kuirithi mikoba ya Smith pale Villa Park.

Villa wameamua kutafuta suluhisho na kuleta mabadiliko chanya kwenye kikosi chao kutokana na kukaa nafasi ya 16 baada ya michezo 12 ya Ligi Kuu na wamefikia uamuzi wa kumfuta kazi Smith baada ya kupoteza katika michezo mitano mfululizo ya ligi.

Terry alichaguliwa kuwa kocha msaidizi wa Smith mwaka 2018 na kuisaidia Villa kupanda Ligi Kuu na aliachana na timu hiyo msimu uliopita wa majira ya joto.

Gerrard kwa sasa ni kocha mkuu wa Rangers ambaye amewapa taji la Ligi Kuu ya Scotland kwa mara ya kwanza, yupo kwenye mkataba na klabu hiyo hadi mwaka 2024.



# Jones awindwa na timu 13

**LONDON,** England

LICHA ya kuwa nje ya uwanja kwenye kikosi cha kwanza cha Manchester United kwa muda mrefu, Phil Jones anahusishwa na klabu 13 zinazohitaji huduma yake.

Jones anatakriban miaka miwili hajaingia kwenye kikosi cha kwanza cha 'Mashetani Wekundu' hao kutokana na kupata majeraha.

Kwa sasa amerejea mazoezini na amecheza michezo kadhaa ya wachezaji wa chini ya umri wa miaka 23 kama sehemu ya kurejesha kiwango chake.

Klabu kadhaa zimekuwa zikimtaka Jones tangu majira ya kiangazi, lakini kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer amekuwa akizuia usajili wake akiamini kuwa, anaweza kuwa na msaada ndani ya kikosi chake.

Miongoni mwa klabu hizo 13 ni pamoja na Watford na Newcastle United ambazo zinatajwa kuisaka saini ya Jones kwa mkataba wa mkopo.

Timu zingine zinazoiwania sahihi ya Jones zinatoka Championship ikiwamo Derby County inayonolewa na Wayne Rooney.



HABARI MICHEZO


7,771,400 JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/11/21 | 18:00 | Rochdale vs Leyton Orient | 2.27 | 3.28 | 2.99 |
| 02. 13/11/21 | 18:00 | Tranmere vs Sutton United | 2.32 | 3.23 | 2.94 |
| 03. 13/11/21 | 18:00 | Stevenage vs Mansfield | 2.46 | 3.20 | 2.76 |
| 04. 13/11/21 | 18:00 | Bristol Rovers vs Northampton | 2.41 | 3.19 | 2.85 |
| 05. 13/11/21 | 18:00 | Walsall vs Harrogate | 2.60 | 3.23 | 2.60 |
| 06. 13/11/21 | 18:00 | Altrincham vs Boreham Wood | 2.83 | 3.27 | 2.35 |
| 07. 13/11/21 | 18:00 | Yeovil vs Eastleigh | 2.38 | 3.22 | 2.83 |
| 08. 13/11/21 | 18:00 | Wealdstone vs Barnet | 2.43 | 3.41 | 2.63 |
| 09. 13/11/21 | 18:00 | Accrington vs Plymouth | 2.70 | 3.44 | 2.39 |
| 10. 13/11/21 | 20:15 | Mirandes vs Huesca | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 11. 14/11/21 | 18:00 | UD Ibiza Eivissa vs Almeria | 3.13 | 3.18 | 2.24 |
| 12. 14/11/21 | 20:15 | Leganes vs Real Oviedo | 2.29 | 2.99 | 3.23 |
| 13. 14/11/21 | 20:15 | Burgos vs Ponferradina | 2.41 | 3.03 | 2.98 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 11 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1233 | Chiangmai United vs Khon Kaen United FC | 2.05 | 3.42 | 3.13 |
| 14:00 | 3471 | South Korea vs United Arab Emirates | 1.35 | 4.06 | 8.70 |
| 15:00 | 1341 | Port FC vs Ratchaburi | 1.67 | 3.61 | 4.43 |
| 15:00 | 3806 | Macedonia U21 vs Ukraine U21 | 3.38 | 3.24 | 2.02 |
| 15:00 | 4033 | Lebanon vs Iran | 9.44 | 4.05 | 1.34 |
| 15:00 | 4425 | Vietnam vs Japan | 14.40 | 6.15 | 1.15 |
| 16:00 | 1877 | Tanzania vs DR Congo | 2.85 | 2.99 | 2.41 |
| 16:00 | 4513 | Uganda vs Kenya | 1.61 | 3.42 | 5.39 |
| 16:00 | 4988 | Ethiopia vs Ghana | 9.67 | 4.45 | 1.30 |
| 17:00 | 3031 | Baumit Jablonec vs Varnsdorf | 1.24 | 5.79 | 8.49 |
| 17:00 | 3851 | Maccabi Kishronot Hadera W vs MS Kiryat Gat W | 5.57 | 4.61 | 1.42 |
| 18:00 | 2373 | China vs Oman | 2.70 | 3.09 | 2.46 |
| 19:00 | 1411 | Malaga C.atco W vs Prainsa Zaragoza W | 2.05 | 3.48 | 3.09 |
| 19:00 | 2818 | Benin vs Madagascar | 1.55 | 3.56 | 5.77 |
| 19:00 | 5259 | Congo vs Namibia | 1.98 | 3.13 | 3.61 |
| 19:00 | 5745 | Rwanda vs Mali | 5.20 | 3.32 | 1.65 |
| 20:00 | 1377 | Iraq vs Syrian Arab Republic | 2.08 | 2.99 | 3.52 |
| 20:00 | 1758 | Croatia U21 vs Estonia U21 | 1.01 | 15.45 | 97.56 |
| 20:00 | 2242 | Armenia vs North Macedonia | 2.85 | 3.30 | 2.46 |
| 20:00 | 3625 | Georgia vs Sweden | 7.22 | 4.11 | 1.47 |
| 20:00 | 4163 | Azerbaijan vs Luxembourg | 2.50 | 3.05 | 3.00 |
| 20:00 | 4407 | Serbia vs Qatar | 1.49 | 4.20 | 6.60 |
| 20:00 | 5308 | Russia vs Cyprus | 1.15 | 7.23 | 18.07 |
| 20:30 | 1827 | Ukraine vs Bulgaria | 1.58 | 3.94 | 5.79 |
| 20:30 | 3369 | Hapoel Nir Ramat Hasharon W vs Bnot Netanya W | 1.17 | 7.14 | 9.65 |
| 20:30 | 3386 | Czech Republic vs Kuwait | 1.30 | 5.40 | 9.41 |
| 20:45 | 1267 | Hapoel Raanana W vs Hapoel Beer Sheva W | 1.71 | 3.96 | 3.81 |
| 21:00 | 3739 | San Marino U21 vs Israel U21 | 87.03 | 15.47 | 1.01 |
| 21:30 | 2923 | San Martin Burzaco vs CA Atlas | 2.46 | 3.04 | 2.75 |
| 21:30 | 3541 | Hapoel Marmorek Rehovot vs AS Tel Aviv University W | 15.41 | 9.25 | 1.08 |
| 21:30 | 4119 | El Porvenir vs Lujan | 2.28 | 2.89 | 3.17 |
| 21:30 | 5459 | Leandro N Alem vs Claypole | 3.12 | 2.59 | 2.54 |
| 22:00 | 2549 | England U21 vs Czech Republic U21 | 1.50 | 3.96 | 5.60 |
| 22:00 | 3974 | Togo vs Senegal | 5.77 | 3.41 | 1.58 |
| 22:00 | 4527 | Hungary U19 vs Italy U19 | 5.41 | 4.35 | 1.46 |
| 22:00 | 4893 | South Africa vs Zimbabwe | 1.31 | 4.43 | 9.05 |
| 22:45 | 3180 | Malta vs Croatia | 22.96 | 8.19 | 1.12 |
| 22:45 | 3765 | Greece vs Spain | 7.42 | 4.21 | 1.45 |
| 22:45 | 3843 | Germany vs Liechtenstein | 1.03 | 13.29 | 59.80 |
| 22:45 | 4181 | France U21 vs Armenia U21 | 1.01 | 15.49 | 77.46 |
| 22:45 | 4426 | Slovakia vs Slovenia | 2.19 | 3.05 | 3.64 |
| 22:45 | 4508 | Ireland vs Portugal | 8.61 | 4.91 | 1.35 |
| 22:45 | 4828 | Romania vs Iceland | 1.60 | 3.90 | 5.60 |
| IJUMAA - 12 - NOVEMBA 2021 | | | | | |
| 00:00 | 5963 | Ecuador vs Venezuela | 1.39 | 4.50 | 8.41 |
| 01:00 | 2359 | Ponte Preta vs Botafogo RJ | 2.85 | 2.99 | 2.41 |
| 01:00 | 2386 | Flamengo vs Bahia BA | 1.39 | 4.43 | 6.55 |
| 01:00 | 3237 | Sampaio MA vs Vila Nova GO | 2.95 | 2.90 | 2.41 |
| 02:00 | 1738 | Paraguay vs Chile | 2.58 | 3.03 | 2.93 |
| 03:00 | 1370 | Estudiantes Rio Cuarto vs Temperley | 2.31 | 2.79 | 3.23 |
| 03:30 | 1763 | Brazil vs Colombia | 1.46 | 4.29 | 7.18 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# WENGER AJUTIA KUCHELEWA KUONDOKA ARSENAL



**LONDON,** England

ARSENE Wenger anajutia kung'ang'ania kubaki kwenye Klabu ya Arsenal baada ya kuondoka kwa uchungu msimu wake wa mwisho mwaka 2018.

Wenger mwenye umri wa miaka 72, aliitumikia klabu ya Arsenal kwa muda wa miaka 22 na kuiongoza kutwaa mataji matatu ya Ligi Kuu England na mataji saba ya Kombe la Ligi, FA.

Kuna makala imeandaliwa ya msimu wa 2003/04 ambayo imepewa jina la "Arsene Wenger: Invincibles" na inatarajiwa kutoka wiki hii na kuonyeshwa kwenye kumbi mbalimbali za sinema.

Wenger ameweka wazi kuwa ilibidi aondoke Arsenal miaka kumi iliyopita, wakati anahitajika na klabu nyingi pamoja na timu za taifa.

Wenger amesema, "muda mwingine nashang'aa, kuna kitu nilikosea baada ya msimu wa "Invincible" 2003/04?

"Mwaka 2007 ulikuwa ni wa maamuzi, ni kwa mara ya kwanza nilihisi kuwa kuna msukumo mkubwa ndani ya bodi, ilikuwa nichague kuwa mwaminifu kwa klabu au vinginevyo.



# Yorke: United inaweza kutwaa ubingwa EPL

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Dwight Yorke, anaamini kikosi hicho chini ya kocha Ole Gunnar Solskjaer kinauwezo wa kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu England.

Mchezaji huyo wa zamani kutoka Trinidad & Tobago anaamini kikosi cha Man United kimesheheni wachezaji wenye ubora unaoweza kuwafanya kushindana na timu zinazowania ubingwa wa Ligi Kuu England, huku akisisitiza kuwa ina viungo wazuri zaidi ya Liverpool.

"Nadhani tuna wachezaji wanaoweza kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu England, je, wanacheza kama mabingwa? Hapana, tukirudi nyuma misimu mitatu au minne wakati Leicester City wanachukua ubingwa, unaweza kuona wachezaji waliokuwa nao na wachezaji tulionao sisi, tuna wachezaji wazuri wanaoweza kuchukua ubingwa," alisema akinukuliwa na BT Sport.

"Tuna kikosi kizuri, tuna walinzi imara, tuna golikipa bora na washambuliaji hatari, watu wanazungumza kuhusu viungo, huwezi kuwa na timu iliyokamilika.

"Huhitaji kuwa na kikosi kilichokamilika ili uweze kchukua ubingwa, ila unahitaji watu wanaoweza kubadilisha matokeo na kutawala mchezo, tuna Cristiano Ronaldo, Edinson Cavani, Paul Pogba na Raphael Varane ni uwendawazimu kuona nafasi tulipo, ni kweli inavunja moyo kuangalia na ni ngumu kukubali pia."

Man United watarudi tena uwanjani baada ya mapumziko ya kimataifa na kusafiri kwenda kucheza na Watford Novemba 20, mwaka huu.

# Michezo

Alhamisi Novemba 11, 2021

Nipashe




Xavi aunda jopo lake, atimua wa2

UKURASA 21

NIMEWASILI...




Kocha Mkuu mpya wa Simba, Mhispania Pablo Franco baada ya kuwasili Dar es Salaam jana tayari kwa kuanza kuwanoa mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA: SIMBA**

## Franco 'awasapraizi' Simba akiwasili Dar

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Kocha Mkuu mpya wa Simba, Mhispania Pablo Franco Martin, 'amewasapraizi' mashabiki wa timu hiyo, baada ya mpango wa kuwasili kwake Dar es Salaam jana kufanya kimyakimya na uongozi wa klabu hiyo.

Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, juzi alimwambia mwandishi wetu kuwa Franco atatua siku yoyote wiki hii bila kuitaja na aliendelea kusisitiza hivyo kwa vyombo vyote vya habari nchini kila alipoulizwa, kabla ya jana asubuhi kocha huyo kutua nchini kuchukua rasmi nafasi ya Mfaransa Didier Gomes ambaye alitangaza kubwaga manyanga, baada ya timu hiyo kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy mwezi uliopita.

Mtandao rasmi wa klabu hiyo ulionyesha video fupi ya kocha huyo akipokewa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere na Mratibu wa Klabu ya Simba, Abasi Ally, akiwa wakala wake raia wa Kenya.

Franco hakuwa na mengi ya kuzungumza zaidi ya kuongea maneno mawili ya kiswahili "pole pole, hakuna matata," alipoulizwa kama anafahamu kiswahili walau kidogo.

Kocha huyo ambaye amewahi kuwa kocha msaidizi wa Real Madrid mwaka 2018 huku pia akiinoa Getafe ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kabla ya kutua Simba alikuwa akiifundsha Klabu ya Al Qadsia ya Kuwait kuanzia mwaka 2019 hadi 2021.

# Stars: Safari Kombe la Dunia ni leo

**Na Saada Akida**

### ●●● Poulsen asema hakuna namna ni ushindi tu kwa Mkapa, wachezaji mzuka juu, Hector Cuper aonya...

LICHA ya kuwa vinara wa Kundi J, kwenye mechi za kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar, hakuna namna ya kujihakikishia kutinga mechi ya mwisho ya mchujo pasipo kupata ushindi leo dhidi ya DR Congo katika mchezo utakapopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa timu Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Kim Poulsen.

**Tanzania inaongoza Kundi J ikiwa na pointi saba sawa na Benin ambayo ipo nyuma yake kutokana na tofauti ya mabao ya kufunga, huku DR Congo ikifuata kwa alama tano na Madagascara ikiburuza mkia kwa pointi tatu.**

Timu itakayoongoza katika kila kundi kati ya 10, itachezeshwa droo ili kucheza mechi ya mchujo nyumbani na ugenini na tano zitakazopata matokeo ya jumla zitaliwakilisha Bara la Afrika katika michuano hiyo mwakani nchini Qatar.

Hata hivyo, Taifa Stars inashuka uwanjani leo kuikabili DR Congo ikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya bao 1-1 timu hizo zilipokutana nchini Congo katika mchezo wa awali, shukrani kwa Simon Msuva aliyeifungia kwenye mechi hiyo akisawazisha bao la Dieumerci Mbokani.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, kuelekea mchezo huo wa leo, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Kim Poulsen, alisema wako tayari kwa ajili ya mchezo huo na lengo lao ni kumaliza hatua hii ya makundi wakiwa vinara wa Kundi J.

"Tunawaheshimu DRC ni timu nzuri, najua wamekuja hapa kwa ajili ya kuharibu mipango yetu, lakini naamini wachezaji wataweza kukamilisha mipango yetu.

"Tunafurahi kesho (leo) tutakuwa mbele ya mashabiki wetu ambao wamekuwa nasi kuanzia mwanzo hadi sasa katika mchezo huu, tutaingia [uwanjani] kivingne tofauti na ule wa awali," alisema Poulsen.

Alisema anawashukuru wadhamini wakuu, serikali na mashabiki ambao wako nyuma yao wakiwapa sapoti wakati wote.

Naye nahodha msaidizi wa Taifa Stars, John Bocco, alisema maandalizi kuelekea mchezo huo ni mazuri na wako tayari kwa ajili ya mchezo huo na wanaimani wanaenda kushinda.

"Tunaingia katika mchezo huu tukiwaheshimu DRC, ni timu kubwa lakini tunawaomba mashabiki wetu watuombee, tunaamini tunaenda kupata matokeo," alisema Bocco.

Kocha Mkuu wa DRC, Muargentina Hector Cuper, alisema itakuwa mechi ngumu, lakini lengo lao ni kupata ushindi ingawa wanajua haitakuwa rahisi kutokana na aina ya wapinzani wao.

"Tuna wachezaji wengi wanaocheza nchi mbalimbali ikiwamo England, lakini hapa tunaangalia ubora wa timu nzima si mchezaji mmoja mmoja, naamini tutapata matokeo," alisema Cuper.

Nahodha wa DRC, Mbokani alisema hawana presha na wako tayari kwa ajili ya mchezo huo na lengo lao ni kushinda ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kukamilisha ratiba.

"Katika nafasi tuliyopo, tunatakiwa kushinda ili kujiweka katika mazingira mazuri ya mchezo wa mwisho dhidi ya Benin," alisema Mbokani.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >